EGLISE DE LA SAINTE FAMILLE
EN AFRIQUE

A. S. B. L.

JAMAA TAKATIFU MU AFRIKA

Siège Social : Kalemie
B.P. 77
KALEMIE

# KATEKISMU YA KANISA LA JAMAA TAKATIFU MU AFRIKA

E. S. AF./J. T. AF.
LUBUMBASHI — AOUT 1984

**EGLISE DE LA SAINTE FAMILLE**
**EN AFRIQUE**

A. S. B. L.

**JAMAA TAKATIFU MU AFRIKA**

Siège Social : Kalemie
B.P. 77
KALEMIE

# KATEKISMU YA KANISA
# LA
# JAMAA TAKATIFU MU AFRIKA

Kwa baba Professeur Johannes FABIAN,
Zawadi ya wababa na wamama
wa J.T.AF.
Lubumbashi, le 13/07/1986
Mchungaji Mkuu

EGLISE DE LA SAINTE FAMILLE EN AFRIQUE
E.S.AF - J.T.AF
SIEGE SOCIAL
B.P.77 KALEMIE
JAMAA TAKATIFU MU AFRIKA

LU[illegible]EMA KAPITENI

E. S. AF./ J. T. AF.
LUBUMBASHI — AOUT 1984

==================================================

Kitabu hiki cha KATEKISMU kimetungwa na Mchungaji Mkuu LUTEMA KAPIFENI, akisaidiwa na Comité Central ya Kalemie,

na

kikakubaliwa na Assemblée Generale ya Zaïre.

==================================================

Kalemie, août 1983.

ooooOoooo

# U T A N G U L I Z I

==========================

Kitabu hiki kidogo ni msaada kwa wa Pasteurs na waamini wetu wa kila Station na kila Section, ili wawe na kitabu kwa kutambulisha kile watakuwa nafanya mbele ya waamini na Mungu. Kitabu hiki ni mwangaza wa wote, kwa wababa na wamama waliokwisha kupata mafundisho mengi, na hasa kwa waumini wapya.

Ni hivi ndani ya kitabu hiki muna mawazo yafuatayo :

I.- Imani yetu ya JAMAA
II.- Mafundisho ya wenyi kutaka UBATIZO
III.- Mafundisho ya KOMUNYO YA KWANZA
IV.- Mafundisho ya UCHUMBA
V.- Mafundisho ya watoto wadogo na vijana
VI.- MASHAURI ya wazazi kwa watoto wetu.-

Kanisa inaomba kila muongozi atumie kitabu hiki kwa uaminifu mkubwa ndani mwa Bwana Yesu na Mama Bikira Maria.

oooOooo

# I N G I L I O.

====================

Kuhusu mwendo wa Imani yetu ni kubwa; kwa sababu huyu Yesu na Maria tunaowasadiki si mfano wa mbali: Yesu ni NENO lenyewe la Mungu. Neno ndiye amejifanya MTU. Neno halikufika duniani kwa mfano wa Mungu, bali limefika kama mtu. Kumbe mtu huyu aliahidiwa na Mungu mwenyewe tangu zamani za kale -MIKA 5:2-5.

Kumbe mwanamke aliyetumiwa ni yule yule ISHARA - UFUNUO 12:1-6. Na sisi kama tuko ndani ya nyumba, baba na mama, ni kwepesi kujua kama Mungu alijifanya MTOTO ndani mwa muke. <u>Hakuna dunia bila mama kuwa ako</u> na <u>hakuna dunia bila mwanaume kuwa ako</u>.

Kanisa letu ni MAMA WA MAKANISA YOTE, kwa sababu kila Kanisa munaingia watu wawili tu (2): bibi na bwana. Na wanamutaja Yesu ndani ya kila Kanisa; Mama Maria wanaye kwa fumbo tu. Na mama ndani ya nyumba ndiye mfano wa Maria. Tunawaharifu kama tuheshimu watu wote wa makanisa yote iliyo ulimwenguni, kwa sababu Maria mwenyewe amesema kama vizazi vyote wataniita mwenyi heri - LUKA 1:46-49; ISAYA 7:10-14.

Tena kwa upande wa Imani, tunaisha kuonyesha kila njia Imani yenyewe ya Yesu na Maria: <u>Imani katika maisha mapya</u>, <u>Imani katika kuamini kwetu</u>, <u>Imani namna ya wewe kujitazama ginsi uko unaishi na kutunza Imani yako</u>.

Tena tunapenda WALIMU na wa PASTEURS wetu wazidi sana kusoma mambo ya Imani: kile kilichoweza kuleta uharibifu katika JAMAA ni <u>KUKOSA IMANI</u>.

+‡+

Kipindi cha kwanza

# I M A N I   Y E T U   N I   G A N I ?

## Sura ya kwanza : IMANI YETU NI YESU NA MARIA.-

Kuamini kwetu Yesu na Maria kuko natuonyesha njia yenyi kuwa wazi kwa kuendelea na Kanisa letu bila kuchoka katika Imani, sababu Yesu ndiye NENO -YOANE 1:1-18. Pasipo yeye hakukufanyika hata kitu kimoja. Yeye alipofika, akatosha giza. Yeye ndiye asili ya Imani yote ya wenyi kuamini -WAEBRANIA 12:2; akawa na Kanisa Jangwani (MATENDO 7:38-39), akapokea maneno ya uzima atupatie sisi; akaonyesha wazi kama "zamani muliabudu bila kujua, sasa nafika ili muabudu katika ukweli (YOANE 4:21-24).
Ushuhuda wake unapita wa Yoane (YOANE 5:36). Ushuhuda huo ukaongezeka wakati Mitume walipokuwa nyumbani (MATENDO 2:22-41).

Ikiwa tunatambua wazi kama Yesu ndiye Neno, Neno lilikuwa kwa Mungu, likajifanya MTU duniani. Mbele ya kujifanya mtu, alama ilionek na mbinguni (UFUNUO 12:1-6): mwanamke mwenyi kuvikwa nyota kumi na mbili, ufalme wote una yeye; Mungu mwenyi kupenda ulimwengu akatuma mjumbe Gabrieli kusudi ya kumpasha mama huyu atakayezaa Mkombozi wa ulimwengu mzima (LUKA 1:26-38). Mambo ni wazi ya kama sababu ya Maria, watu wote wanakombolewa (MATAYO 1:21) na yeye mwenyewe Maria akasema wazi kama Mungu anapenda kweli kijakazi chake, kumbe vizazi vyote vitaniita mwenyi heri (LUKA 1:46-49).

Leo hatuwezi kupenda Yesu bila kupenda Maria, hatuwezi kupenda kunywa maji na kukataa chura anayebaki ndani ya maji; kiisha unasifu maji. Wokovu ni wazi: kujuwa kama Maria amekuwa mu mawazo ya Mungu tangu zamani. Tazama Nabii Isaya aliyeonyeshwa na Mungu anatabiri wazi (ISAYA 7:10-14; 9:1-3; 54:5-7; MATAYO 1:22-23).

Ukiona mambo haya, ni wazi kama Yesu na Maria ndiyo walio mfano mkubwa wa ukombozi. Na hivi na sisi wenyi kufuata mfano huo, Kanisa la Yesu na Maria ndiyo Kanisa kubwa lenyi kuitwa kama ni MAMA WA MAKANISA (ZABURI IO5:12-16). Walio wachache na kiisha wamekuwa kundi nzima kwa mipaka ya dunia yote; na sisi leo, japo tuko kidogo, na kiisha tutakuwa watu wengi na mwisho mpaka dunia

itambue. Hata tukisema Kanisa hiyo ya Jamaa Takatifu ni mama wa makanisa, mambo yako wazi: sababu Yesu na Maria ndio walituma Mitume; ni katika umoja wao wa tangu pa Nazarethi Yesu alituma Mitume (MATAYO 28:17-20); mwisho akawashuhidia Roho Mtakatifu (MATENDO 1:4-5). Kumbe kama ni yeye aliyewatuma, na anatutuma na sisi tutangaze habari yake na tuzidi kumushuhudia kama vile Yoane alimushuhudia (YOANE 1:19-34).

.../...

## SURA YA PILI : ALAMA YA MSALABA NA SALA.-

Katika Imani hatuna mashaka tena sababu Yesu mwenyewe tunamujuwa na tuko hakika kwa mambo yote tunayoenda nayo (WAEBRANIA 11:1; MATENDO 10:20).

Kwa upande wengine, Kanisa inatuonya wazi kama hatuwezi tena kupiga ALAMA YA MSALABA. Neno "alama" ni kama mtu mwenyi kuheshimu kivuli; halafu yeye mwenyewe hajioni umtu wake (I WAKORINTO 1:18-31). Tukichunga "alama" tutakuwa sawa Wayunani, ni kukosa majibu yetu mbele ya Mungu aliyetufia msalabani. Sisi inafaa tuchunge msalaba (GALATIA 2:20). Hata na katika maandiko, Yesu mwenyewe anasema wazi kama "chugua msalaba wako, unifuate" (MATAYO 10:34-39). Hakusema "chugua alama yako" ! Inafaa tufahamu msalaba wa kweli: ni makosa yako ile Baana Yesu aliyofia, ni matendo yako.

Kwa Imani yetu, tunawaonya kama vile Maria ni Ishara na kiisha kuonekana duniani, alipokea salamu kutoka kwa Malaika Gabrieli. Salamu ile ikawa sala tulipewa zamani na Kanisa tulikuwa nayo. Kwa sasa hatuwezi kulinda tena salamu ile kama sala kwetu; sisi tunapashwa sasa kumsifu Maria. Salamu inahakikisha kama mtoto ndiye atakuwa mkubwa wa watu wote, na ni yeye Mtoto wa Aliye juu.

Kufuatana na kuitika kwa Maria, inaonekana kama shetani aliangushwa. Kumbe ni bure kutoa tena salamu ama "jambo" kila wakati, ila kusifu tu (LUKA 1:39-49). Kwa Imani yetu, tunaongeza tena kama sala ya Kumsifu Maria tusali hivi :

"Maria Mtakatifu Mama wa Yesu uliyemkanyaga shetani kwa nguvu ya Mungu Baba
- Uishi kati yetu kama vile pa Nazarethi, ukituombea daima kwa Yesu wako, atupe Uzima, Uzazi na Mapendo." -

Tukiendelea na mawazo haya ya Imani yetu, ifuatayo ni sala ya Baba yetu, iliyofundishwa na Yesu Kristu wakati bado angali duniani pamoja na Mitume wake. Wanafunzi wake walipomuuliza kama "Bwana, utufundishe ginsi ya kuomba: Tutaomba namna gani ?" Yesu alijibu: "Ombeni Baba yenu aliye binguni." Sisi wa J[illegible], Sala hii isaliwe vile iko ndani ya Biblia (M.T.YO 6:9-15) :

"Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litakaswe, ufalme wako uje, mape zi yako yatimizwe hapa duniani kama huko mbinguni ..
- Utupe siku kwa siku riziki yetu. Utusamehe zambi zetu kwa kuwa sisi nasi tumsamehe kila anaye tukosea. Na usitutie majaribuni, lakini utuopowe na yule muovu." -

Kwa Imani yetu, Sala ya Sifa tusome LUK. 2:14-20. Hatuwezi kuendelea na sala "vile Mungu alikuwa mwanzo": Mungu, mwanzo, aliazibu dunia na akaihurumia. Kumbe sasa TUMSIFU, TUMUABUDU NA TUMSHUKURU. Kwa sababu Majusi walipofika mbele yake, walimuabudu, walimsifu na walimshukuru (LUK. 2:20-21). Hatuwezi kurudia ku maneno ya mwanzo, sababu mwanzo Mungu aliazibu dunia; kwa kuonyesha kama yeye ni Mungu wa huruma, aliahidia kama hataazibu tena dunia hata kidogo (MWANZO 8:21-22).

Kumbe ni vile tunapashwa kujua wazi kama Mungu ni mwingi wa rehema, tunaadiki kila siku na kila wakati wa maisha yetu duniani (ZABURI 65:1-4). Tena Imani yote imeletwa na yeye (LUK. 2:13-14). Sala ya Sifa ni hii :

"Sifa kwa Mungu juu mbinguni na amani duniani kwa watu wenyi mapenzi mema -
- Tunakusifu, tunakuabudu na tunakushukuru."-

.../...

SURA YA TATU : MAJIFU NA MAJIVI.-

Kwa Imani yetu, tukifuata mawazo ya kama sisi ni udongo (Majifu), miaka iliyopita tulipakaliwa majifu ya miti; lakini mawazo haya yalionyesha nini katika maisha ya mwanadamu ?(YOANE 3:5-6). Yesu anatafuta mtu upya: alisafisha hekalu, alisema nini ? Alisema kama hekalu ilikuwa nini ? Alisema kama hekalu ni mwili wa mtu mzima (YOANE 2:12-25). Hivi kama mawazo ya ndani

inaharibika, mwili wote mzima si safi tena. Kumbe Yesu alitaka watu wawe safi kwa moyo. Hivi tunatambua kama mwili wetu ni mwili mtukufu kwa sasa, hasa kwa yule mwenyi kujitambua kama Kristu alifufia msalabani (I WAKORINTO 3:16-17). Hivi tuliumbwa kwa udongo na tutarudi kwa udongo, tutagusa udongo pahali pa kupakaliwa majifu (MWANZO 3:19). Sababu mtu alipokosa, aliumbwa na Mungu kama wewe u mavumbi na utarudi mavumbi (MWANZO 3:19-20).

Kwa Imani yetu, zamani kiisha kubariki matawi, mulikuwa nabeba matawi na kwenda nayo nyumbani kwenu. Lakini sasa, kiisha kubariki matawi, mutakuwa nalacha ndani ya Kanisa (MATAYO 21: 1-9). Wakati huo, kiisha kumshangilia Yesu, hakuna mtu aliyerudia na mitende ya miti.

Kwa siku ya leo, tutakuwa kabila moja: maneno haya yamehidiwa wazi na Yesu mwenyewe (YOANE 10:15-16). Maandiko yanasema wazi kama Yesu ni wa wote (MATENDO 2:39-40). Kufuatana na kutawanyishwa na kufukuzwa kwa leo, tuko na yule anaye tukutanisha (YEREMIA 23:1-8). Kwa Imani tunainua Kanisa letu kama yile makanisa yote, tukifuata mfano wa wale watu wa mbele walioinuliwa na Mungu (WAEBRANIA 11:1-40). Kumbe kwa sasa tutahesabiwa kwa Imani (WARUMI 3:27-30). Kwa upendo wake busio na mipaka aliumba mtu kwa sura na mfano wake (MWANZO 1:26). Ndiyo sababu Kanisa letu, inafaa kila mtu ajuwe kama cha lazima ni kuwa na Imani ya kupenda kila mtu, kwa sababu ni sura na mfano wa Mungu. Tena Mungu, japo tulimkosea, tuko sura na mfano wake (MWANZO 9:6). Yeye wa uwezo alitupidia ukombozi (MIKA 5:2-5).

Ni hivi tunapashwa kusadiki kama ukombozi umetimilika siku Yesu alisema: "Yote yamemalizika."(YOANE 19:30). Kama Yesu alikufa kwa ajili ya watu wote duniani, ni katika jina na njia ya Kristu tumepata amani ya ndani ya moyo.-

\+ +

SURA YA INE : UJIMA - UZAZI - UPENDO.

Tazama zamani Mungu aliyekuwa rafiki wa Ibrahimu, wa Yakobo na Musa, amekuwa Mungu wa wanadamu wote kwa upanga aliokuwa katikati ya Mungu na watu na uliofunguka kwa alama ya pazia la hekalu liliopasuka vipande viwili toka juu hata chini pa kufa kwa Kristu (MARKO 15:38).

Hivi sisi Waafrika tuna kitu katika maisha yetu. Ndiyo maana hata tulifundishwa elimu nyingi kutoka kwa wazungu (Ulaya), tuna kitu (LUKA 19:26). Yesu anasema "Kila mtu aliye na kitu atapewa, lakini yeye asiye na kitu, hata kile anacho atanyanganywa."

Kwa Imani, tunawaonya kama sisi watu tuna mawazo matatu: <u>Uzima</u>, <u>Uzazi</u> na <u>Mapendo</u>. Na haya tulioonyesha. Na kama hayapo ndani mwa mtu wako, unakuwa mtu-nyama ama mtu-udongo, mwenyi kupenda kufikiri juu ya maisha ya mwili watu tu na kunywa, basi. Hapa ukiwa hivi, kiisha kupoteza mawazo haya yote, unakuwa <u>udongo mtupu</u> (I WAKORINTO 15:39-41; WAEFESO 2:1-2). Pa nafasi hii Imani yetu ni yenyi kufa: haitaweza kufahamu kitu tena utakuwa nafanya hapa chini ya jua.

-/-

## SURA YA TANO : MTU NI MFANO WA MUNGU.

Ingawa mtu mtu ana cheo kikuu miongoni mwa viumbe, yeye pia ni udongo: Mungu alimuumba kwa mavumbi ya inchi (MWANZO 2:7).

Kuhusu mtu kama udongo, tazama AYUBU 10:9;33:6;34:15; ZABURI 90:3;104:29; MUHUBIRI 3:20;12:7; ISAYA 64:8; WARUMI 9:21; I WAKORINTO 15:47. Ni hivi, wazazi, picha ya mtu kila siku inaelekea uharibifu, tafauti kati ya Mungu na mtu: <u>Mungu ni Mungu</u> na <u>mwanadamu ni mwanadamu</u>. Lakini inafaa mwanadamu kumcha Mungu Muumbaji wake kwa unyenyekevu. Hatari tuko nayo sisi watu ni kujisahau ya kwamba sisi tuko udongo. Lakini tusisahau kama picha yetu ni ya lazima: uharibifu upate kufika ni mwendo wa dunia; wengine wanapenda kujiweka kama wamungu.

Hapa tunaona mfano wa Mungu, maana yake aliumbwa kwa kuishi katika ushirikiano na urafiki na Mungu. Hii ndiyo shabaa kuu ya kuumbwa kwa mtu. Kwa ushirikiano huu, mtu ana cheo kikuu miongoni mwa viumbe vyote. Ni hapa tunapata uwezo wa kutawala viumbe vyote. Kama leo mukitawaliwa na <u>pombe</u>, <u>wizi</u>, <u>uongo</u>, <u>chuki</u>, <u>usharati</u>, <u>matetano</u>, <u>hasira</u> na <u>fitina</u> ndani ya mioyo yenu, mukiwa na matendo haya, hamuko viumbe vyenyi bei mbele ya Mungu, kufuatana na hali Mungu aliwaumba kwa sura na mfano wake (MWANZO 1:26-27). Kumbe kufuatana na mawazo yetu ya J....., haifai baba, mama, kaka ao dada atawaliwe tena na vitu vya dunia, sababu vyote ni vitu sisi tunapashwa kuvitawala.

SURA YA SITA : IMANI NA MAISHA MAPYA

Neno Imani halitumiki katika Agano la Kale, ila mahali pachache sana. Lakini wazo lenyewe lipo mfano mzuri hapa: ni Ibrahimu na habari yake alipokuwa akitoka katika makao yake ya zamani na kwenda fasi asipofahamu (MWANZO 12:1-4; WAEBRANIA 11:8).

Tukizani mfano tunao, tumaanesabiwa kama watoto wa Ibrahimu. Imani hii inaonekana kama wazo la kumtii Mungu kusudi ya kupeana Agano na kwa kulinda uwaminifu na Mungu na mapenzi yake (WAEBRANIA 11:1). Ndiyo sababu kama lec tunasadiki Yesu na Maria, hawaonekane. Lakini inafaa tufuate mfano ule wa Ibrahimu, na katika kusadiki, akapewa Agano, na yote aliyoagana na Mungu yametimilika.

Kumbe nyinyi walimu wote, mumekwisha kuitwa sasa na Mungu kama vile Ibrahimu aliitwa. Haifai tena kuongoza watu kwa kinywa chako, bali kwa kuona kama uko mwenyi kuitwa. Hivi leo tunakuwa na mawazo yetu ya kujitegemea ni vizuri kabisa.

SURA YA SABA : KUAMINI KWETU

1.- Kufuatana na kuamini kwetu Yesu na Maria, siyo mambo mapya ao ya kuiga. Tukifuata mu Agano Jipya, neno "imani" ama kuamini utumika sana, ikiwa na maana mbali mbali.

Mfano : - Wengine wanaamini Mitume
- " " Roho Mtakatifu
- " " Moyo Mtakatifu wa Yesu.

Ndiyo sababu kuamini ni kuamanisha, kukubali yaliyosemwa na Yesu ama Maandiko Matakatifu (YOANE 2:22;3:1.;8:45). Haifai tulinde imani kama Mayaudi waliokuwa na mashaka kila siku.

2.- Maana ya imani ni kumtegemea Yesu ama Mungu katika hatari na mahitaji mbali mbali (MATAYO 8:10;9:1; MATENDO 27:25). Kwetu sisi inafaa tuwe na imani kubwa kwa kulinda Kanisa letu.

3.- Wazo la imani inahusu wokovu wenyi kuwa katika Yesu Kristu. Kwa mfano mkubwa tunaukuta hasa kwa Yoane na Paulo: Paulo anasema kama mwenyi kuamini ana uzima wa milele; Yoane anasema kama ni kumpokea Yesu Kristu. Mara moja moja mu Agano Jipya, imani inajulikana kama karama ya kweli ya kuweza kutenda nayo miujiza (I WAKORINTO 12:9).

Kumbe tunapenda katika Kanisa letu, kila mmoja awe na karama yake, lakini wote tuwe na shirika la kujenga katika Umoja.

## SURA YA NNE : UJITAZAME KAMA UNA IMANI

Kufuatana na mawazo yote, tunawaonya juu ya Imani: ni mambo munapashwa kufuata kwa karibu sana. Sababu kwa mkristu, Ibada na mikutano yaweza kufafanushwa na hali ya pétrole. Hatari yenyi kuwa hapa ni ya kukaa na kuamini, kujuwa maisha ya kila siku: ku Kanisa uko Malaikâ, lakini ku nyumba uko kama shetani. Hapa ni kukosa kujua majibu yako mbele ya Mungu.

Ni hivi tunasema kama Mungu ana ngalia matendo yako, kadiri uko unamkana (TITO 1:16). Ao utaamini kwa kupata uzima wa milele ? Imani nzima inaonekana katika maisha yote: ku kazi, ku nyumba, mu safari. Imani nzima inaza matunda (MATAYO 7:16-17; YAKOBO 2:14-26). Hatuwezi kujaza Kanisa na matendo yasiyofaa. Katika Imani, tusaidiane pia. Mwenyi kuwa katika Imani ni baba na mama wapya katika Kanisa letu, ndani mwa Yesu Kristu (II WAKORINTO 5:17; GALATIA 6:15).

Hatupendi tena ubaya na umama wa zamani kwa sababu ile neno kutahiriwa ni neno nzima. Zamani Mayaudi walikuwa natahiriwa, lakini kiisha Yesu Kristu kuzalika, ilionekana neno la bure. Ndiyo sababu Kanisa inasemakama haifai mtu wa kusema:"Aa mimi ndimi nilimuena Placido": ile haijakuwa neno; neno ni kugeuka mupya na kumuelekea Kristu.

### WAZO LA MWISHO

Kanisa haipingi mafundisho yote tuliyosikia, ila inapenda mutunze Kanisa lenu munale kubwa, kwa sababu leo tunakuwa na manyumba ya kukutana, siyo jambo la kuleta fujo na magombano. Ila Kanisa inawaomba WALIMU, WA PASTEURS, WA SUPERVISEURS, MCHUNGAJI MKUU, MSHUHUDA, tusome YOANE 4:21-23: tukiwa na Imani, hatutakuwa na magumu kwa Kanisa letu .-

KIPINDI CHA PILI

# M A F U N D I S H O   Y A   U B A T I Z O .

## INGILIO

Mwendo wa sisi waAfrika kumjua Mungu, hatukupewa habari na mtu yeyote. Tumemjua Mungu namna isiyosikilika, sababu mpaka leo hatuna maandiko inayoshuhudia kama waAfrika walimjua Mungu kwa upande wa Nabii fulani. Kwa wazungu ni vile: kwao walipokea Manabii (ISAYA I:2-4; YEREMIA I:I5-I9; EZEKIELI 2:I-IO).

Hapa inaonekana kweli ukomo wa Mungu kwa kutuma manabii alitambua kama kabila la Israeli walikuwa watu wenyi kukosa masikio ya ndani; hivi Mungu akawaonya ku njia ya manabii. Imeonekana wazi wakati Mungu alimuita Musa: alipoona chicha la moto, Musa hakumjua wazi Mungu (KUTOKA 3:I3-I7).

WaAfrika wote tulimjua Mungu, wala hakukuwa lazima yoyote ya kuuliza mtu. Imetukia pia hata na leo, wakati wa kupigia mzimu, wanataja mzimu na kuunga pamoja na jina la Mungu. Mungu alijulikana kwetu sisi waAfrika kwa njia hiyo; Ndiyo sababu tukifundisha watu hatuna lazima ya kusema mingi zaidi; mawazo yetu hasa tunastahili kutoa ni

- Kusikilizana: hii ni mapashwa yetu sisi waAfrika.
- Kusaidiana : ni mapashwa kwetu; inatokia hasa wakati wa magumu.
- Mapendo : japo ni amri mupya Yesu alipana, lakini kwetu siyo amri mupya, hiyo ni mapashwa yetu kwa maisha yetu ya kila siku.
- Hekima : ndio msaada wa sisi waAfrika Mungu aliotupatia kwa kushauria hata mtu asiyemujua.

Kiisha tutaongeza na mawazo ya kitabu cha MWANZO na vile tutafikia ku Agano Jipya, pia na ku Ndoa.

## I.- MUSIKILIZANO.

Kufuatana na hali yetu, mawazo juu ya <u>musikilizano</u> ni mawazo mazuri. Nayo kwetu ni mapashwa ya tangu asili ya wakambo wetu; pia na mambo haya yalikuwa ku Israeli (MWANZO 31:43-55). Tunakuta Yakobo mwenyi kupatana na Labano. Mbele ya kupatana kwao, kulikuwa kitu ama alama, kijulisho kwa masikilizano: ni <u>jiwe</u>. Halafu mababu waAfrika walifanya nini ? Kwa kusikilizana, waliweka kitu kati yao; hasa walikuwa natumia JIWE ao MZIZI ao KUKATA LITETE ao LIKAA YA MOTO, kiisha wanaizima mbele ya watu wote. Ndiyo ilikuwa alama ya watu kusikilizana.

Mara ingine walikuwa natumia majani ya mti "kifumbe": kiisha kuchugua majani ya mti ule, mtu yule wa kusema anaweka lijani lile ku kinywa, kiisha anaanza kusema, akitafuna pole pole.

Tena kuhusu musikilizano katika Agano Jipya, Yesu mwenyewe ameunganisha waSamaria na Mayaudi (YOANE 4:9,39-42): watu hawa hawakuwa napatana, lakini wamepatana siku ile.

Kama musikilizano ni mapashwa yetu, ndiyo maana tunasema kama JAMAA ni Kanisa la MUSIKILIZANO, MUSAIDIANO na MAPENDO. mawazo haya matatu ukiyashika, utakuwa mkristu mwema ndani ya J.T.AF.

- Siyo musikilizano wa dunia kama wandumba,
- siyo musikilizano wa kundi la kazi la ma ofisa fulani,
- siyo musikilizano wa makundi ya dunia tunayoona.

Mungu mwenyewe ni asili ya musikilizano wa ndani. Kumbe kila baba na mama ajuwe kama musikilizano ndiyo msinji wa JAMAA: nyumbani kama hamuna musikilizano, hamuna Mungu hata kidogo.

## II.- MUSAIDIANO.

Ikiwa kama tulisikia mawazo juu ya musikilizano, ndiyo kiini cha kwanza, kwani watu wakisikilizana, mwisho watasaidiana kwa kila kitu. Lakini kufuatana na musikilizano, kama kuna musikilizano wa kila namna, ndiyo maana pa musaidiano wako, inafaa uwe na moyo ule ule ulikuwa na muSamaria mwema (LUKA 10:30-37): Huyu alisaidia bila kuangalia kama huyu ni ndugu yangu ao anipe faida; alimfanyizia tu kwa moyo mwema, pia na moyo wa huruma (MATAYO 5:7).

Kumbe kwa kusaidiana mu nyumba baba na mama, sherti kuwa na moyo wa huruma: ukihurumia baba ao mama, ni kwepesi kumsaidia kazi anayo. Kwetu sisi haifai kusahau kama, kwa asili yetu, mtu akifika ku nyumba ao ku mgini fulani, wale wenyi nyumba ao mgini wanatayarisha chakula na kumupa ale ao anaweza kupewa kipande cha shamba alime. Musaidiano ni mapashwa yetu katika magumu, hasa mu mgini mukifa mtu, siku ile hakuikalake mtu wa kwenda ku shamba ao ku kazi fulani: ilikuwa mpaka wazike mt , kiisha ndiyo wanafanya malazima yao. Kumbe musaidiano ni mapashwa ya tangu mababu wetu wa sisi waAfrika.

Tena juu ya musaidiano, ni jamb lililoonekana wazi kwa Yusufu: japo ndugu zake walimuuzisha ku utumwa, wakati chakula kilikosa katika inchi yote, alisaidia ndugu zake wakati alipokuwa ku Misri (MWANZO 44:1-33).
Bila kusahau, sisi wazazi tusiwe na musaidiano wa deni ao kusaidia tu rafiki wako ao yule mwenyi kukusaidiaka kila mara katika maisha yako. Inafaa tusaidie na adui, bila kusahau kama musaidiano tunafanya ni ule wa Mungu wa kusaidia watu na ku roho (EZEKIELI 3:16-21).

## III.- MAPENDO.

Mapendo ndiyo amri ya mwisho na ni amri kubwa, ginsi Yesu alivyosema wazi katika Agano Jipya (MATAYO 22:36-40). Mu Agano la Kale, mababu walijuwa kama mapendo ndiyo asili ya kuvunja vitu vyote: hasira na chuki (WALAWI 19:18). Mababu wa huku Afrika waliweza pia kuonya mawazo juu ya mapendo: mtu hasiyekuwa na mapendo walisema kila mara "<u>ni mlozi</u>", kufuatana na amri hiyo ya mapendo. Ni hivi ilikuwa zamani mtu katika kutembea kwake walikuwa natembea na vitu vitatu ndani ya "<u>lindo</u>"yake: barua ya njia, barua ya kumaliza mashamba na barua ama cheti cha mganga. Mulikuwa pia buku ya palata.




1= Mukaba wa kubebea
2= Mufuniko wa lindo
3= Fasi ya kufungia lindo
4= Lindo lenyewe

Mtu akiwa na vitu hivi ine ndani ya lindo lake atatembea bila magumu. Lakini watu wa wakati huo hawakuwa na feza ama makuta, walikuwa nakula nini ? Walikuwa napokelewa kila fasi kwa ajili ya mapendo

Tufuate mfano wa Yesu kwa sababu Mungu amemtuma Yesu mwenyewe kusudi ya kutuokoa (I YOANE 4:7-24). Kama Yesu amejitolea kwetu, kumbe kati yetu tusiwe tena na wazo mbaya; kukiwa wazo mbaya, mapendo haitakuwa safi tena (WARUMI I3:8-IO^. Mapendo inavunja yote, hata kukiwa mtu mwenyi nia mbaya juu yako, ukiwa na mapendo, hawezi kitu (WARUMI 8:3I-39). Ndiyo maana Kanisa letu, nguvu yake ni mapendo, hasa baba na mama nyumbani: haifai kuwa na mapendo mpaka kama baba ao mama anakutimilizia vile unapenda. Mapendo ya Kanisa letu ni Yesu na Maria. Mapendo ya Mungu siyo ya kuchora na ukorofi wa asili ya matendo mabaya: mapendo ifuatane vile JAMAA imekuwa pale mwanzo. Mufahamu nyinyi wenyewe ndani ya JAMAA: waongozi walisema sana juu mapendo, lakini ilionekana kama mapendo ilikuwa tu juu ya chakula (ugali, wali wa ku shangwe).

Tujikaze kupendana kusudi tutimize amri kubwa ya mwisho; nayo ndiyo inafunga umtu wetu na kutugeuza tuwe watu wapya.-

## IV.- MASHAURI YA HEKIMA.

### UTANGULIZI

Kama hivi leo tuko watu tunakaa pamoja, kusali na kujua kama siku moja tutakufa na tutaenda mbinguni. Kwa sasa mbingu haionekane, lakini hapa tuko naona dunia. Basi nani alituzaa mu dunia ? Ni baba na mama. Kumbe yatupasa kuheshimu baba na mama ambao tunaishi nao (MEZALI I:8); bila kusahau kama inafaa vile vile kuheshimu wakubwa wa Kanisa na Serkali, ndiyo pahali pa wazazi wetu wa roho. Na itakuwa kwepesi kuungana na Mungu.

### 1)- MAONYO MBALI MBALI

Kawaida yetu, mara nyingi sisi waAfrika tulipata magumu hasa kwa ajili ya kinywa chetu sisi wenyewe: ukiwa muongo ao mtu wa kusema mingi, wa hasira, wa fitina, watu wa mgini hawatakupenda hata kidogo. Kumbe hapa inafaa kuwa mtu wa kujiokoa: usitoe ulimi kwa maneno maovu, hasa kwa wageni (MEZALI 6:I-5). Ukiwa mtu wa fujo, unajitia mu mtego kila mara na mu hasara kwa upande wa maisha yako.

2)- MWENYI AKILI NA MJINGA

Kufuatana na hali yetu ya kiAfrika, mtu akifa, ilikuwa lazima kutafuta "Alikufa nini ?" Hapa lifo kingine kinatambulikana na kwa matendo: kama mtu akifa vibaya, walijuwa namna ya magonjwa yake: mara kusemasema pa kufa na kulalamika.Ndiyo sababu kila neno inafaa kuwa na woga, kwa sababu ukitenda kila neno kwa ujeuri,yule aliye kuumba anakutazama; ukijitisha mu dunia, anaona vyote. Kumbe ukiwa na woga, utakuwa pia na ufahamu na akili ya kimungu (MEZALI 9:IO-I2).

3)- MATUNDA YA HAKI NA YA UOVU

Tukiangalia mwendo wa watu, inaonekana wazi mtu mzuri kila siku anatumainiwa na watu wote; ila mtu mbaya naye kila siku na kila wakati matendo yake hayafichame. Kwa hivi tunapenda Kanisani mwetu tupendane wote, tuwe watu wazuri kusudi tuwe na matendo ya kupendeza (MEZALI I2:I-9).

Ukipenda mashauri, utakuwa mtu mwema; na kama hausikie mashauri, uko kama nyama. Mtu mzuri anakubaliwa na Mungu kwa matendo yake, mpaka akapate faida mbele ya Mungu.

4)- TAFAUTI KATI YA AKILI NA UJINGA

Kufuatana pia na kawaida ya sisi watu wa Afrika, hakuna mtu mwenyi kupenda fujo, ila fujo inatokana na Shetani.Ndiyo maana ukipenda kuwa mtu mzima, toa maneno ya kutuliza, utajenga kila mara (MEZALI I5:I-4). Ukiwa na sauti nzuri, ni kwepesi kugeuza mtu wa hasira. Tena ulimi wa mtu mzuri unatosha maneno mazuri; lakini mupumbafu hana maneno mazima.Ndiyo sababu Mungu yuko naona yote tunayofanya. Ulimi njo uzima wa mtu (YAKOBO 3:I-I2).

5)- HEKIMA YA MTU MZURI

Nyinyi kama munapenda kubatizwa, ni vizuri. Lakini inafaa kujua kama kuisha kubatizwa, kyenyi kuombwa ni matendo na mifano yenu, ndiyo vitavuta watu na kuwazaa (MEZALI II:30). Ni vile kama nyinyi munabatizwa, munakuwa watu wa kuleta uzima ku watu wengine munaoishi nao.

6)- MAFUNDISHO KWA MTU WA MUNGU

Tukiwafundisha siyo sababu ya kubatizwa na kiisha munabakia mu matendo ile mulikuwa nayo zamani, kwa sababu zamani mulipenda kuishi fasi ya pombe (MEZALI 23:3I-32), michezo isiyofaa, kukaa katika vikundi vya kila namna, haifai, kwani kila kundi ina msemeo wake na ule msemeo ukiwa nao pamoja, utakitia mu hasara (MEZALI 24:I-2): iwezekana je wewe pusi ukae pamoja na mbuzi ? Usipoangalia vizuri utatoa mulio wa mbuzi ! Muko naona vile dunia iko mpaka leo: mtu mwengine anaweza kutoa maneno aliyosikia tu kwa mwengine, kiisha maneno yale inakuwa yake. Si mbali kabisa, hamujaona mtu akienda kuangalia mchezo wa kabumbu, japo hacheze, kama kabumbu inaingia mu nyavu, watu wote wanaruka na kufurahi pamoja na wachezaji ? (MEZALI 24:25-26).

7)- NAMNA YA KUPATA HEKIMA

Wazo la mwisho: kiisha kupata neema inafaa itumike, kwa sababu mafundisho yote tunaisha pata hapa, hata mababu wetu waliweza kuletewa mawazo haya, ni vile iko na leo. Choyo siyo asili yetu ao kutumikisha mtu na kumunyima haki yake siyo sawa. Na kama mtu anakosewa, wewe ukiwa na kitu na unakataa kumpatia, hiyo siyo sawa (MEZALI 3:27-28).

Kuhusu mawazo yenyi kuelekea heshima, kwa kuwa heshima njo hali ya kiAfrika, haikuwa lazima ifundishwe; ile ni kazi ya kila mtu mweusi: alipewa kutenda hivi ni vizuri na hivi ni mubaya. Basi ilikuwa inatukia hata mtu akifanya vibaya, mababu wanamuonya ginsi ya kuishi kama mtu mkamilifu katika maisha yake.

8)- KAZI YENYEWE

a) KUUMBWA KWA ULIMWENGU.-

Ulimwengu humu tunamokaa ni inchi Mungu alituumbia ili tuishi kwa mapendo makubwa. Vile Mungu yuko mwenyi kutupenda sana, amefanya kwanza vyote vya lazima (MWANZO I:I-25). Na mwisho alitoa kile kiumbe kyenyi bei kubwa: njo wewe baba na mama. Akatufanya nyuma ya vyote (MWANZO I:26-3I).

MWALIMU : aonyeshe wale wa Ubatizo ginsi Mungu aliseza kufanya kazi hiyo ya kuumba mtu wake. Mungu ni mkamilifu na kwa ukamilifu huu anamaliza kazi yote ya kuumba ulimwengu ni kwa ajili yako wewe baba na mama.

b) EDENI.-

Mtu aliumbwa vema bila taka lolote, mwenyi sifa na uwezo, mtu wa ukweli na mwenyi haki; akawekewa fasi nzuri sana. Mtu huyu aliyeumbwa alipewa mawazo matatu: UZIMA - UZAZI - MAPENDO. Mawazo haya yalimusukuma mtu kijiona kama yeye mwenyewe si mkamilifu, ni mwenyi kukoswa kitu. Basi alijiona UPEKE (MWANZO 2:2I-25).

MWALIMU : ajulishe wazi kile kilimuwazisha Adami ni nini ? Njo Umtu. Sasa hapa kusudi la Mungu linaonyesha kama mtu hawezi kuishi peke yake, anapewa bibi. Kama leo unabatizwa, sherti uchunge mawazo yale matatu ya Uzima, Uzazi na Mapendo.

9)- UBATIZO NI TENDO LA TANGU ZAMANI

Wakati makohani waliwekwa katika Agano la Kale, walitawaswa kabisa ndani ya maji (KUTOKA 29:4). Yoane Mbatizaji alibatiza wale waliotubu katika maji (LUKA 3:7-8). Tena alionyesha kama ukohani wa zamani za kale uliishawekwa kando (WAEBRANIA 7:I2). Ndio maana wakristu wote ni makohani (I PETRO 2:5-9; UFUNUO I:5-6, 9-I0). Bwana Yesu Kristu, Kohani mkubwa, alibatizwa ndani ya maji na Yoane (MATAYO 3:I3-I7). Ni hivi Bwana Yesu aliahidi kama wakristu wote wanapashwa kubatizwa (MATAYO 28:I9; MARKO I6:I6). Kubatizwa ni kawaida na kunaonyesha kama unavaa Kristu (GALATIA 3:27). Tena Ubatizo ni mfano ya wokovu toka tufani kuu, Ubatizo ukiingiza mtu chomboni mwa Noa na Ubatizo ni jibu ya zamiri safi mbele ya Mungu (I PETRO 3:20-2I).

Hiyo yote inaonyesha hivi:

- Ubatizo unasafisha uchafu wa roho, sio wa mwili (I PETRO 3:2I);
- Ubatizo ni kwa wao wenyi moyo safi mbele ya Mungu(I PETRO 3:2I);
- Tena Ubatizo unaonyesha wengine ya kuwa zambi zetu imeisha kusamehewa (MATENDO 2:38; 22:I6);
- Tena Ubatizo ni kwa wale walioisha amini na moyo woye juu ya Bwana Yesu (MATENDO 8:36-37).

Ubatizo ni mfano wa kuzika maisha ya zamani na kuanza maisha mapya katika Bwana Yesu (WARUMI 6:I-5; KOLOSAYO 2:I2). Tukiangalia YOANE 3:5. neno maji halihusu Ubatizo; maji ni neno la Mungu linalosaidia mtu kuzaliwa mara ya pili (YOANE I5:3; WAEFESO 5:26; YAKOBO I:I8; I PETRO I:23).

Kumbe kwa upande wetu, hatuwezi kubatiza watoto wachanga kwa sababu watoto wachanga ni bora kuwawekea mikono tu hekaluni (MATAYO I9:I3-I5) kwani ufalme wa mbingu ni wao (MARKO IO:I4).

**MWALIMU** : aonyeshe kile kinaleta Ubatizo.

Kufuatana na mawazo ya kuumbwa kwa mtu, vile tumewafasiria kama ameumbwa vizuri na Mungu, sasa mtu kwa kiburi chake amekosa (MWANZO 3:I-2I). Kwa kosa hili tumefika wote mu zambi ya asili. Ni kule sasa kunatufikia tubatizwe ili tuzalike mara ya pili (YOANE 3:I-7). Kumbe nyinyi munataka kuzaliwa mara ya pili na ni pale sasa mutageuka kuwa watoto wa Mungu. Na kiisha kubatizwa, munapata uzima wa milele (YOANE 3:I5).

MWALIMU : Kazi kubwa sasa ni kujikaza kutenga uzima wa mwili na uzima wa roho, ili mtu ajuwe kama maisha ya mwanadamu yeyote ina uzima mbili: uzima wa mwili na ule wa roho.

## IO)- KUTUBU NA IMANI VINATEMBEA PAMOJA

Ukipenda kusamehewa zambi zako, Yesu ndiye aliyepewa na Baba yake uwezo wa kuondoa zambi (MATENDO 5:3I). Kumbe na nyinyi mumtegemee Yesu Kristu. Ni yeye mwenyi uwezo wote. Manabii walimshuhudia kama yeye Yesu ukimwamini, utapewa msamaa wa zambi zako (MATENDO IO:43). Mambo hayo yanatukia wazi. Na wakati Kornelio alipotubu, amebatizwa pamoja na ndugu zake (MATENDO IO:45-48). Wokovu ni kwa kila mtu mwenyi kuamini Kristu, na ndiye anayestaili kubatizwa kwa jina la Yesu Kristu.

MWALIMU : awaonye kama kiisha kupata ubatizo, wanaanza tangu saa ile kazi, kwa sababu mgeni hasiyejuwa kanuni ya mgini hana hukumu yake, lakini mwenyi mgini ni mwenyi kujuwa [illegible] yote: akikosa, hukumu yake ni kubwa sana. Njo kama nyinyi wanao batizwa: ukikosa, hukumu yako ni mbali mbali na mpagani (WARUMI 2:2-5). Hapo inaombwa ukijua ubaya, usiufanye wala usihukumu na kurazau wema Mungu alikupa kiisha kuzaliwa kwako kama mtu mupya; inafaa kuchunga ile zawadi atakuletea siku ya Ubatizo wako.

11)- KWA KUPOKEA UZIMA WA MILELE

MWALIMU : Kupokea kitu ni kusadiki na kuamini kama vile nyinyi munaamini na kutubu: uzima umefika kwenu (MATENDO II:I8 YOANE 5:24).

SHIKA UKWELI:

Mafundisho tunayowapatia, muyashike na kuyalinda, ni ile itawasaidia kwa kusema ukweli, ni ile itageuza matendo yenu na kuonekana kama mupo wenyi kubatizwa na Mungu (2 TIMOTEO 2:I5; YOANE 5:39; MATENDO I7:II).

I2)- MALAIKA NI MJUMBE WA MUNGU

Kufuatana na maisha ya mwanadamu, ameumbwa kwa mfano wa Mungu. Na njia moja Mungu anatuletea Malaika wa kutuangalia ginsi tuko mu nyumba bibi na bwana: bwana ni Malaika mlinzi wa bibi na bibi ni Malaika mlinzi wa bwana (I KORINTO II:IO; 4:9; I TIMOTEO 5:2I).

Tena Malaika wana furaha kubwa kama sisi watu wote tuko wenyi kuokoka (LUKA I5:IO). Hasa Malaika njo wachungaji wa watu (DANIELI 6:22).

Tena mukisha kubatizwa, haifai kupiga watoto wenu ao kuwakosea, kwa sababu wao pia wana Malaika sawa na wewe mtu mkubwa (MATAYO I8:IO).

MWALIMU : Malaika katika kuchunga kwao wanachunga zaidi watu wenyi kuamini Kristu (MATENDO 27:25; LUKA 22:43; MWANZO I9). Kumbe mujikaze kuchunga mawazo kila wakati ili Malaika apate kuwachunga.

I3)- MALAIKA WABAYA

Malaika mubaya alifungwa kwa hukumu ya mwisho (YUDA I:6; 2 PETRO 2:4). Munasikia hapa na inaonekana wazi kama Mungu ni mwenyi uwezo mkubwa, ginsi ametendea Malaika ingawa ni roho tupu. Halafu wewe kiumbe una nguvu gani ? Kumbe inafaa tuogope Mungu !

PEPO WACHAFU WATAISHI NDANI YA MWILI WETU

---

MWALIMU : ukaze mawazo haya.-

Mtu akiachana na mwenyi kumchunga analiwa na KIMBULU, kimuzimu. Mkristu akiachana na Mungu anaweza kupata pepo mbaya (MARKO 5:2; LUKA II:I4). Lakini mkristu wa kweli anaweza kufukuza pepo mu jina la Yesu Kristu (MARKO I6). Na wale wasioamini hawawezi kuwafukuza wale pepo wabaya (MATENDO I9:I3-I7).

MWALIMU : uzidi kufahamisha ya kama Yesu hakuja kama Neno, ila alibeba mwili wa mtu. Mpaka leo kunakuwa kila mtu anapenda kuombea watu. Je ? wakati unaenda kuombea mgonjwa ao mwenyi pepo, unajuwa ana nguvu gani ? Haifai kusikia tu kama waliombea mtu fulani, hivi na wewe unakuwa mkristu, unaweza kuombea mtu ! Sivyo.

MWENYI KUPINGA KRISTU

---

Kufuatana na maisha ya ulimwengu, kuko watu wenyi kupinga Kristu. Kiisha Ubatizo wao, watafika nao kujidai kama WA-Kritu (I YOANE 2:I8). Wao wanakataa Kristu aliyeshuka duniani na kutumwa na Baba yake (YOANE 5:43; 2 TESALONIKA 2:8-II; 2 YOANE 7). Mawazo tunawaonya iko hapa duniani. Kumbe hii ni habari ya kuja kwake Mpinga-Kristu (2 TESALONIKA 2:3-II).

* * *

Kufuatana na mawazo tuliowaonya walimu tangu mwanzo wa kitabu hiki ku upande wa Imani yetu, Yesu na Maria ni mawazo yale ya MSIKILIZANO, MSAIDIANO na MAPENDO. Kiisha kuonyesha Hekima ya MEZALI, ile ni njia tuliwapa waumini namna ya wao kusikia sasa Imani ndani ya moyo wao. Mtu hawezi kusikia Imani kama hajakuwa bado na nia ya kusikilizana na watu, kusaidiana nao na kupendana nao. Na mtu hawezi kupokea Imani kama hana Hekima. Akiwa na Hekima, atajuwa kile anachopenda kufanya wakati ule.

Ni hivi tunawajulisha waumini kama Hekima bila Imani ni bure na Imani bila Hekima ni bure; inafaa kuwa na vyote viwili pamoja: Imani na Hekima.

MWALIMU : Kazi kubwa, wewe unaweza kuwa mwalimu, lakini uko unafundisha watu, kila wale wenyi kuwa na madawa ao mizimu. Kwa Imani yako unasema mutoshe mizimu; hapa ujuwe kama mafundisho yako yatakosa bei; mbele umsaidie kwa upole, ndiyo kazi ya Hekima. Na kwa Hekima yako, utamjaza Imani na mwisho utaona atakutolea mizimu ile yuko nayo. Kumbe tufundishe waumini wetu kwa Hekima, na kiisha tutawajaza Imani kubwa.

## I4)- IMANI NI NINI ?

MWALIMU : Imani si kujuwa kanuni pasipo shaka, ila inafaa kujuwa tu kama Mungu yuko (WAEBRANIA II:7; YOANE 20:3I; I YOANE 5:IO). Imani ni kupokea shukrani; karama tunapewa na Mungu (YOANE I:I2).

Mwenyi Imani ya kweli harudi nyuma wala hakani Mungu (WAEBRANIA IO:38-39). Kwa kawaida, kurudi nyuma kuna maana: ulikuwa mkristu, kiisha yake unaacha ukristiani wako: vile si vema. Kama unakuwa na Imani ya kweli, inaongoza mtu kwa kumkiri Yesu Kristu kama ni Mwokozi (WARUMI IO:9). Haifai kuwa na Imani ya kusema "Mimi nilibatizwa": ile haitoshi na haiwezi kukuokoa na hautapata jibu kwa Mungu (YAKOBO 2:I8-20). Imani sharti iwe na matendo, kufuatana na mawazo tuliwapasha juu ya Hekima: mtu wa Hekima ndiye mtu wa matendo mema. Imani inamkaribisha Bwana Yesu kwa kila njia (WARUMI IO:I3).

## IMANI IKO INATUFIKIA TOKA MBINGUNI NAMNA GANI ?

MWALIMU:: Mungu yuko natoa kama zawadi; yeye ndiye anayetusaidia kwa kuamini (YOANE 6:65). Unaona Mungu yuko nasaidia mwanadamu kila siku (WARUMI I2:3; WAEFESO 2:8).

Lakini hatupewe Imani bure, ni kwa njia ya kusikia neno lake na kufika ku Ibada, ku mafundisho (MATENDO 4:4; WARUMI IO:I7). Kama tunabatizwa, asili ya Imani ni Yesu: yeye njo yuko natupatia Imani (WAEBRANIA I2:2). Haifai kuangaika na madawa. Imani ni tunda linalozaliwa na roho yetu (I KORINTO I2:9). Wazo kubwa ni kupendana kati yenu, kuvumiliana mu nyumba pia na mu Kanisa kwa kila mwamini wetu; musidi kubebana.

TUNAWEZA KUPOKEA IMANI NAMNA GANI ?

MWALIMU : Tunaweza kuipokea na kutumia Imani kama tuko tayari kwa kusikia na kutii neno la Mungu (MATENDO I6:3I-32). Haifai kusikia mafundisho bila kuiweka ndani ya moyo wako, utakuwa nafanya kazi ya bure (WAEFESO I:I3). Mumeitwa na kutiwa muhuri. Imani tunaipokea kasa tena kwa njia ya maombi.

MAWAZO YENYI KUZUIA IMANI

MWALIMU : Kanisa letu ni la Umoja, Msikilizano, Msaidiana na Mapendo. Ikiwa wewe unatafuta sifa, unazuia Imani yako ao Imani yetu ndani ya Kanisa letu (YOANE 5:44), kwani ile sifa ikiwa na mtu mmoja, atapokezana na wengine.

Imani ni kitu kisichoonekana wazi wazi (YOANE 6:30). Wengi siku ile wakashindwa kutambua kile Yesu alikuwa nafanya.

IMANI INALETA NINI ?

MWALIMU : Imani inaleta wokovu (WAEFESO 2:8). Kama Imani inaleta wokovu, haifai kuacha ama kutangana tena na mawazo ya Mungu. Kumbe tunapata uzima wa milele ku njia ya Imani (YOANE 6:47). Na kwa kuwa tunaamini, tujuwe wazi kama uzima wa milele ni kwetu.

Kwa Imani tunapata uwezo wa kuwa wana wa Mungu (GALATIA 3:I6; YOANE I:I2). Kwa Imani tunatakaswa mioyoni mwetu (YOANE I5:3), na tunaweza kukaa na kushiriki pamoja na Mungu, tukiungana naye (2 PETRO I: 4). Na kwa Imani tutapata utakatifu (MATENDO 26:I8) na Kristu atakaa kati yetu (WAEFESO 3:I7); hata kwa hiyo tutapata ruhusa ya kufika mbele ya Mungu wetu (WARUMI 5:2; WAEFESO 3:I2).

Kumbe tunawaonya vile Imani inafanya kazi. Njo sababu kama tunaamini Yesu na Maria, tunastahili kujisifu na kuchunga huyu Yesu mpaka mwisho wa maisha yetu yote hapa chini ya jua.

*   *   *

# MAULIZO NA MAJIBU JUU YA KIPINDI CHA KWANZA NA CHA PILI .

1.- Yesu tunaye amini ni nani mbele ya Mungu Baba ?
JIBU/ Yesu ni Neno (YOANE 1:1-18).

2.- Maria naye ni nani ?
-J/ Maria ni Ishara (UFUNUO 12:1-6).

3.- Nani aliyeleta Msikilizano ?
-J/ Ni Yesu (YOANE 4:9,39-42).

4.- Ni nani aliyesaidia yule mtu aliyepigwa na wanyanganyi ?
-J/ Ni Msamaria mwema (LUKA IO:30- 32).

5.- Ni Nabii gani aliyetumwa na Mungu kusaidia watu kwa upande wa robo ?
-J/ Ni Ezekieli (EZEKIELI 3:16-21).

6.- Amri gani ni kubwa kuliko zote ?
-J/ Ni amri ya mapendo (MATAYO 22:35-40).

## MAULIZO YA HEKIMA.-

7.- Ni mtu gani anayechukiwa na watu ?
-J/ Mtu muovu, muongo na mtu wa fujo (MEZALI 6:1-5).

8.- Wakati wa kufa kwake, mtu mbaya anafanya nini ?
-J/ Analamukalamuka na kusema mingi (MEZALI 9:10-12).

9.- Mu Kanisa letu, mtu mzuri ana faida gani ?
-J/ Anatamaniwa na waumini wote (MEZALI 12:1-9).

10.- Maneno ya mtu mpole inaleta faida gani ?
-J/ Inajenga watu (MEZALI 15:1-4).

11.- Ukiwa na matendo mazuri, wewe uliyebatizwa utaleta nini mbele ya watu ?
-J/ Utavuta watu na kuwazaa (MEZALI 11:30).

12.- Ni vizuri kulewa pombe ?
-J/ Hapana (MEZALI 23:31-32).

13.- Kiisha kubatizwa, tunaweza kuishi katika kila kundi ?
-J, Hapana (MEZALI 24:1-2).

14.- Kwa kulinda hali yetu ya kiAfrika na kupata neema kwa Mungu, yatupasa kuacha nini ?
-J/ Choyo: kumunyima mtu haki yake ao kukataa kumpatia yule anayetaka kile ninacho (MEZALI 3:27-28).

MAULIZO JUU YA :

KUUMBWA KWA ULIMWENGU :

15.- Katika namba ya kuumbwa kwa vitu vya dunia, mtu aliumbwa wa ngapi ?
-J/ Mtu ni kiumbe cha mwisho (MWANZO 1:26-31).

EDENI :

16.- Katika bustani, mtu aliwaza nini ?
-J/ Alijitambua katika Upeke (MWANZO 2:21-25).

UBATIZO - ZAMBI - MALAIKA - MPINGA KRISTU :

17 - Sababu gani tunabatizwa ?
-J/ Kwa sababu tumeriti zambi ya asili (MWANZO 3:1-21).

18.- Kwa Ubatizo, tunazalika mara ngapi ?
-J/ Tunazalika mara ya pili (YOANE 3:1-7).

19.- Nani aliitwa wa kwanza na Mungu ?
-J/ Ni Ibrahimu (MWANZO 12:1-4).

20.- Kuna tafauti **kati ya** kutubu zambi na kuamini ?
-J/ Hakuna, vyote ni pamoja (MATENDO 5:31).

21.- Kwa kupokea uzima wa milele, yatupasa nini ?
-J/ Tusadiki na kutubu (MATENDO 11:18; YOANE 5:24).

22.- Mbele ya Mungu, Malaika ni nani ?
-J/ Malaika ni mjumbe wake (I KORINTO 11:10).

23.- Malaika wanachunga nani ?
-J/ Wanachunga watu wote, zaidi wanachunga wenyi kuamini Kristu (MATENDO 27:23; LUKA 22:43).

24.- Malaika wabaya wanafanyiwa nini na Mungu ?
-J/ Wanafungwa (YUDA 1:6; 2 PETRO 2:4).

25.- Mtu akifa vibaya anaweza kugeuka nani ?
-J/ Anaweza kugeuka kuwa pepo mbaya (MARKO 5:2; LUKA 11:14).

26.- Watu wote wenyi kutaja jina la Kristu ni watu wa Yesu ?
-J/ Hapana, wengine ni wapinga-Kristu (I YOANE 2:18).

MAULIZO NA MAJIBU JUU YA IMANI.
---

27.- Imani ni nini ?
-J/ Imani ni kumjua Mungu (WAEBRANIA 11:7).

28.- Mwenyi Imani ya kweli ataacha tena ?
-J/ Hapana, ataendelea mbele (WAEBRANIA 10:38-39).

29.- Kwa mwenyi Imani, Kristu ni nani ?
-J/ Kristu ni Mwokozi (WARUMI 10:9).

30.- Imani ni kuamini tu ?
-J/ Hapana. Imani ni kuamini na kutenda matendo ya Imani (YAKOBO 2:18-20).

31.- Mwenyi Imani anakaribisha nani nyumbani mwake ?
-J/ Anamkaribisha Kristu (WARUMI 10:13).

32.- Nani anayetusaidia kwa kuamini ?
-J/ Ni Mungu (WARUMI 12:3; WAEFESO 2:8).

33.- Mungu anatusaidia namna gani ?
-J/ Ku njia ya kusikia neno lake (MATENDO 4:4; WARUMI 10:17).

34.- Asili ya Imani ni nani ?
-J/ Ni Yesu (WAEBRANIA 12:2).

35.- Imani yenyewe inaanza namna gani ?
-J/ Ni kama tunda (I KORINTO 12:9).

36.- Tutapokea Imani je ?
-J/ Kwa kusikia neno la Mungu na kutii (MATENDO 16:31-32).

37.- Kitu gani kitakachoweza kuzuia Imani ?
-J/ Sifa na kupokezana maneno ya fujo (YOANE 5:44).

38.- Imani inaleta nini ?
-J/ Imani inaleta wokovu (WAEFESO 2:8).

39.- Tunapata uzima ku njia gani ?
-J/ Ku njia ya kuamini, tunapata uzima wa milele (YOANE 6:47).

* * * * * * *

KIPINDI CHA TATU

## MAFUNDISHO YA KOMONYO YA KWANZA

Yesu ni Mungu Mwana: kama vile mulibatizwa mu jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu, sasa hivi kwa yule hasiye mupokea Kristu, yeye Mwana aliyetumwa na Mungu, moyoni mwake hana uzima ndani mwake (MATENDO 4:I2; I YOANE 5:I2).

Kristu ndiye njia ya kufika kwa Mungu (YOANE I4:6; IO:I,9; WAEFESO 2:I8; WAEBRANIA IO:I9). Naiyo sababu Kristu amefanya mkate siku ya Ine , ili apate kula pamoja na wa Mitume, alama ya umoja, na akasema Mufanye hivi kwa kunikumbuka: na hiyo ni kwa ajili ya kuungana naye (I KORINTO II:23-27).

Kumbe wakati utakackomonika, sadiki kama huyu ni Yesu mwenyewe kwani mwili wetu na roho yetu vinakombolewa na damu yake Kristu (I KORINTO 6:20; MATAYO 8:I7).

JUMA YA KARIBU NA KOMONYO :

MWALIMU : Kuwafundisha toba.-

Inafaa mujue makosa na kutubu (MARKO I:I-4; MATAYO 3:2; 4:I7). Ilikuwa kazi pia ya Yesu kuwaambia wanafunzi wake kutubu (MATAYO 6:I2; LUKA 24:47). Na wao wanafunzi walitabiri pia mawazo ya kutubu (MATENDO 2:38; 20:2I). Kumbe kama unakataa kutubu, hautapokea Yesu, utaangamizwa (LUKA IO:I3; I3:3). Ni Mungu anaagiza watu wote watubu (MATENDO I7:30; 2 PETRO 3:9).

a) KUTUBU KWENYEWE NI NINI ?

- Kutubu ni kugeuza mapenzi yetu juu ya zambi na kuiacha (LUKA I5:I8-20; ZABURI 38:I8).
- Kutubu ni kuonyesha sikitiko juu ya makosa tuliyofanya, kunuzunika (YOELI 2:I2; LUKA I8:I3).
- Kutubu ni kuungama zambi zetu mbele ya Mungu wetu na mbele ya wale tuliowakosea (ZABURI 3I:3-4; YAKOBO 5:I6; MATAYO 5:23; LUKA I5:I8; UFUNUO 2:22; 9:20).

- Kutubu ni kuacha kabisa njia mbaya ya zambi na kumugeukia Mungu na Enjili yake (MATENDO 26:I9; I TESALONIKA I:9; ISAYA 55:7).

Kumbe hivi munaanza kukomonika, mujuwe kama kuna namna ya kutubu; musiwe munapokea Bwana Yesu kama mkate tu na uzuri wa inje tu, hapana ! Bali muupokee kama mwili wa Kristu na divai kama damu yake, mukijuwa kama munameza Kristu mzima.

b) KUTUBU KUNALETA NINI MU MAISHA YA WEWE MWAMINI ?

- Kutubu kunaleta matendo mema (MATAYO 3:8; MATENDO 26:20; UFUNUO 3:5).
- Kutubu kunaleta kusamehewa kwa zambi (LUKA 24:47; MATENDO 3:I9; 5:3I).
- Kutubu kunaleta uzima wa milele (MATENDO II:I8).
- Kutubu kunaleta maarifa ya kweli ya Mungu (2 TIMOTEO 2:25).
- Kutubu kunaleta karama ya Roho Mtakatifu (MATENDO 2:38).
- Kutubu kunaleta utukufu kwa Mungu na furaha mbinguni (UFUNUO I6:9; (LUKA I5:7,I0).-

+++

KIPINDI CHA INE

# M A F U N D I S H O  Y A  U C H U M B A

## UCHUMBA

Si jambo lipya, duniani kote watu wanaoana. Lakini kuoana kwetu kunakuwa mifano mbali mbali: kwa wamoja utaowa mtoto kwa bure bila mali; kwa wengine mtoto anauzishwa na mbuzi pia na Makuta ama feza mingi. Lakini mambo hayo siyo ya zamani kabisa, imetukia hasa tangu mwaka wa 1945 kwa kuuzisha mtoto na kuomba mali mingi. Zamani mababu walikuwa wakiowa kwa mali chache. Kwa mfano:

- Batabwa: ilikuwa mara ingine Franka moja (1Fr) na kulima shamba kidogo.
- Baluba: ilikuwa mbuzi moja ao buchanga, biombela (ya mikuba) ao mtumbwi kwa wale wa karibu na maji; na siku hizi, makila.
- Babangubangu: ilikuwa bunduki ya pupu, mushale, kujenga nyumba, maliba (raphia), kibuyu ya mafuta.
- Bahemba: ilikuwa mbuzi mbili, kibuyu ya mafuta, mushale, kisu (lwilu ama faucille mu kifransa), jembe, maliba, vilago viwili na pombe.
- Basonge na Baelande: ilikuwa hasa mafuta na pombe, kilonda ama ndombe (shoka kidogo), na kasolo(kabengele).

Lakini kiisha yake, kufuatana na tamaa ya mali, kila fasi kukazidishwa vitu: mbuzi ikawa fasi ingine kumi na vilago kumi na koti ya baba mzazi na bulangeti. Ku Batabwa ikawa lazima kutoa ngombe na kwenda kulimia baba mukwe shamba munene sana. Burundi, desturi yao ni ngombe tangu asili yao, na leo hii inaendelea, wakitoa ngombe nyingi karibu tano ao sita.

Basi kuoana ilikuwa mfano mbali mbali. Lakini kuoana kwa sasa na kwa zamani kuko mbali mbali, kwa sababu zamani ni wazazi wa mtoto mwanaume wanaenda kumtafutia mtoto wao bibi. Lakini tangu mwaka wa 1960 haikuwa tena vile, hata leo: watu sasa wanaoana mu njia, hata inatukia kijana na binti wanasikilizana njiani, japo wazazi hawajajuwa. Basi kuoana kwa namna hii tutasema kama ni vibaya ao ni vizuri ? Kwa upande wetu, tunaona kama silo kosa la watoto: hapa wazazi wengi hatuna tena mashauri ya watoto wetu kama mababu.

Mbele ya kuwafundisha, kutolewe ulizo, kwani kuoana ni shauri ya watu wawili. Ikiwa kama tunakuja wote wawili hapa, tuko nyumba mbili mbali mbali, kwani wewe baba uko wa nyumba moja na una wazazi wako, na pia huyu mama ni wa nyumba ingine na ana wazazi wake. Basi ukomo wenu wa kufika hapa ni gani ? Munatafuta nini ?
- Wajibu wao wenyewe.-

Kiisha kujibu:"NI VEMA KABISA VIJANA WENU, tunafurahi kuwapokea ndani ya chumba hiki cha mafundisho ya wachumba ili mutayarishe jamaa yenu !"

Basi Mungu tangu mwanzo alisema:" Si vema mtu awe peke yake." Ni hivi akamfanyia msaidizi wa kufanana naye. Kwa hiyo mume atamwacha baba yake na mama yake, naye ataambatana na mke wake, nao watakuwa mwili moja (MWANZO 2:I8-24). Ukomo wa Mungu kwa kufanya hivi ni sababu yeye mwenyewe ni Jamaa na anapenda mtu naye awe na Jamaa wake kama yeye.

MWALIMU : uwafundishe wachumba hawa kipindi cha kwanza cha Jamaa.-

Bwana Yesu mwenyewe akasema wazi kwamba "Hamukusoma kama yeye aliyewaumba mwanzo, aliwaumba mume na mke ?" Basi alisema kwa sababu hiyo: mtu atamuacha baba yake na mama yake, ataambatana na mke, nao wawili watakuwa mwili moja; hata wamekuwa wawili, si wawili tena, bali mwili moja; Mungu aliwaunganisha, mwanadamu asiwatenganishe (MATAYO I9:4-6).

MWALIMU : aonyeshe kama maadui wa ndoa ni watu wa dunia, marafiki na wandugu wa bwana.-

Furaha yenu ni hapa, lakini kiisha ikiwezekana, mutachungu-liwa kama mulisikia maana ya ndoa yenyewe. Baadaye uwaongezee kipindi cha pili cha Jamaa ku wa Malaika. Ginsi kila mtu alipewa Malaika mlinzi wa kumchunga duniani, vivyo hivyo na nyinyi mutaanza kuchungana: baba amuchunge mama na mama pia amuchunge baba. Wazo kubwa ni kushauriana na kusikilizana mawazo, pia muliyopokea ku wazazi wenu. Pa nafasi hii, mutakaa pamoja, hakutakuwa mzazi wa mmoja wenu atakayesema: "Mwende mukapigane ao ukamtakie mwenzako mabaya." Hayo ni mawazo ya tangu zamani, kila mara watu pa kuchu-mbiana wanapewa mashauri ya kuchungana (MWANZO 24:58-60).

Kwenu mukienda kukosa masikilizano, masaidiano na mapendo, umbali mbali utaenda kuingia mu nyumba yenu.

MWALIMU : uwafundishe kipindi cha Malaika kwa kujuwa kama kila mtu ndani ya nyumba ni mlinzi wa mwenzake.

MWALIMU . uwafundishe mafundisho pa kipindi cha Jamaa pa Nazarethi: vile Yozefu na Maria walisikilizana na kusaidiana na kupendana, inaombwa vile vile waume wapende wake wao kama Kristu alivyopenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yetu; vivyo hivyo imewapasa waume wapende wake wao kama vile miili yao wenyewe (WAEFESO 5:25-28). Mume ampende na kumpa mke wake haki yake na mke ampe mume wake haki yake.-

MWALIMU : aangazie vijana hawa ya kwamba mke hana amri juu ya mwili wake, bali mume, na mume vile vile hana amri juu ya mwili wake, bali muke. Mke na mume wawe na masikilizano ya kuenea, ili musinyimane isipokuwa nyinyi wenyewe mupatane kwa muda, lakini mupatane kwa siku zote, kwa kupata furaha ya kusali ao kufunga, kiisha mukajuane tena, Shetani hasije kuwajaribu kwa kutokuwa na kiasi ku nyumba yenu (1 KORINTO 7:3-5). Nyumba yenu iwe katika amani.-

MWALIMU : uwafundishe vijana hawa kipindi cha ine cha Jamaa ku wa Mitume, kusudi wakaishi kama askari wa kweli wa Bwana Yesu na kumuzalia Kristu watoto wa roho.

Itakuwa vizuri sana kama mama anakuwa na mwendo wa utii kwa baba kusudi karibu yao kukiwa watu wasiomujuwa Mungu, wakavutiwe na mwendo wenu. Mama awe mwenyi heshima na asiyekuwa na hofu pia (1 PETRO 3:1-2). Na wewe baba, ukae na mama wako kwa akili na kumupa heshima kama chombo kisicho na nguvu, na kama wariti pamoja neema na uzima, ili hata munapoomba musipate kuzuuliwa (1 PETRO 3:7) na kuvuta wenzenu wengi ndani ya J.T.AF. na Kristu ataishi muzima kati yenu.

UMTU
----

MWALIMU : fanya nguvu ya kuonya vijana ginsi ya kujitambua kati yao, kwa sababu vile tulisema mwanzo kama vijana wengi wanaanza kuoana bila shauri la wazazi, ile ni wazo lilikuwa mbele. Mali ya sisi waAfrika ni miiba: mbele ya kuowa ao ya kuolewa ilikuwa kuuliza kwanza kile kizazi cha wale watu. Njo sababu Mwalimu ajikaze kuwasaidia, ili wasiende kuishi maisha kama nyama; kuwatambulisha kile

kinawaunganishe wawe pamoja ni kitu gani ? Ni
- UZIMA: ndani yake Mungu muna Uzima (YOELI 1:4).
- UZAZI: tazama wana, ndio wariti wa bwana; uzao wa tumbo ni zawabu ao zawadi (MARKO 4:8-9).
- MAPENDO: Kitu kinawela baba na mama mbele yetu kwa kuunga ndoa ni Mapendo. Lakini Mapebdo yenu, mujuwe kama itaisha mu miezi sita tu. Mukipende-nda ku-ishi na Mapendo makubwa, sherti kila mmoja wenu ajitolee kwa mwenzake (1 YOANE 4:7-8).-

MAFUNDISHO YA NDOA

Watu wengi wanafunga ndoa pasipo kujua maana yake na pasipo kujua ya kwamba ni jambo ambalo Mungu aliweka kwa wanadamu uzuri wao. Hivi wawili wasaidiane katika maisha yao. Mungu ni asili ya ndoa; naye anatufundisha namna ya kuifanya vizuri. Tunapashwa kuheshimu ndoa; si kitu cha haya, bali Mungu atahukumu wazini (WAEBRANIA 13:4).

Kwa kawaida mkristu asifanye ndoa na mtu asiyeamini (2 KORINTO 6:14) kwa sababu haifai kuchanga nuru na giza. Kwa sababu ahidi ya Mungu kwanza ilikuwa ya ndoa (MWANZO I:28): zaa watoto. Tena Ishara ya kwanza ya Yesu ilikuwa kwa arusi ya Kana (YOANE 1:11) Mungu Mwenyewe anaunganisha bwana na bibi, si kazi ya mtu tu (MATAYO 19:6). Mtu mkamilifu asiache bibi ao bwana wake na kuowana na mwengine, kwani ndoa ni mpaka kufa (WARUMI 7:I-3). Kwanza kwa usharati anaruhusiwa kumuacha bibi ao bwana yake (MATAYO 5:3I-32); lakini hatari iko: yule aliyeachwa asiolewe wala asiowe tena. Njo sababu kuna wazo la msamaha wa kupokeleana bibi na bwana kusudi wasilete haya juu yao, wasiseme nyuma ya mgongo wao (WAEFESO 5:22-24; KOLOSAYO 3:I8; I PETRO 3:I-6). Kumbe ni bora kuowana katika ubora wote na usafi wote (I TIMOTEO 5:I4; MEZALI I8:I2).

+ + +

## MAELEZO JUU YA NDOA.

Hatuna mawazo mengi ya kuandika juu ya ndoa, sababu ndoa yenyewe huku kwetu Afrika ilijulikana sana. Hakukuwa mtu wa kutesa ama kusumbusha bibi wake wa kwanza. Naye bibi wa kwanza alikuwa anapewa jina kubwa : mara walikuwa wanamuita kwa jina la INABANZA, maana yake "mama wa heshima".

Tena kwa kuweka ndoa ya kweli, waAfrika walikuwa nakunywa damu ya kila mmoja wa wachumba. Iliitwa "LUSALO" : kuchanga damu ya kila mmoja wao, bwana na bibi: huyu anakunywa damu ya mwenzake na mwengine anakunywa vile vile damu ya mwenzake, kila mtu kwa zamu yake. Hiyo ndiyo ilikuwa ndoa ya kweli. Na hakukuwa ginsi ya kuachana mpaka kufa kwao.

*

* * *

*

KIPINDI CHA TANO

# MAFUNDISHO YA WATOTO WADOGO NA VIJANA

SHAURI :

Ndugu Mwalimu wa watoto na Vijana wa JAMAA TAKATIFU, kufuatana na hali ya kujenga Kanisa letu, ni vema zaidi ijitegemee kwa kweli. Kwa sababu Kanisa letu linataka watoto na vijana wetu wote wajuwe Imani (I TIMOTEO 3:14-15). Kwa hivi wengi wetu wameacha Imani hii ya JAMAA na kushindwa kuifuata; haifai tena kuwahesabu kama waJamaa.

Wewe ndugu Mwalimu, ukipenda kujitolea kwa kufundisha watoto na vijana wetu, inafaa ujuwe kama Mungu aliwaita watoto kufanya kazi hii. Hivi wito wa Mungu umetufikia: wengine wameitwa tangu utoto wao (I SAMWELI 3:4-17). Na tena wengine wameitwa wakati wamekuwa watu wakubwa kwa umri kama vile Musa (KUTOKA 3:4-10;11:12;13:16).

Ikiwa leo unakubali kuwa mkombozi wa Kanisa letu, uwe mfano wa Musa: hakuogopa Farao japo alikuwa na kigugumizi (ISAYA 6:5-7; YEREMIA 1:6-10; EZEKIELI 2:6-7; 2 TIMOTEO 1:7; 2:1). Ikiwa wewe ni mwenyi kufundisha watoto na vijana, inafaa kila mara kuungana na Mchungaji ao Msimamizi wa Station ao wa Section kwa kuomba na kupata msaada. Wewe Msimamizi kama unaona kupungukiwa kwa waumini katika Kanisa letu, soma LUKA 10:2.

Katika kipindi hiki tuna sehemu mbili (2):

- Sehemu ya kwanza ni ya Mafundisho ya watoto wadogo tangu miaka sita mpaka miaka kumi na tatu (6-13 ans): tumia picha, kuchora, sanamu, hadisi na nyimbo kwa kuwafundisha. Tena mafundisho isidumu muda mrefu (dakika 30 yatosha kwa somo moja). Tumia njia mbali mbali kwa kuwavuta kama vile chakula, sala, kuwatembelea na kuwapa misaada kidogo kidogo.

- Sehemu ya pili ni ya vijana tangu miaka kumi na ine (I4) mpaka mbele ya kuowa ao kuolewa. Vijana wanapenda kusikilizwa, kuwa-onya, kuwa nao urafiki, kuwatembelea, kuungana nao mu furaha na magumu yao. Tena wewe Mwalimu, uwe mfano mbele yao katika yote na kuishi ujana kama wao. Ukiwa baba ao mama, geuka kijana na kutumia busara.

Mufuate shauri kwa utaratibu.

* * *

SEHEMU YA KWANZA

MAFUNDISHO YA WATOTO WADOGO
( tangu miaka 5 hadi miaka I3).-

SURA YA KWANZA

- KWA JINA ... Maombi ya Mwalimu (iwe inatolewa kila mara mbele ya kuanza mafundisho).
- WIMBO WA FURAHA ... (ule wanajuwa).
- WAZO KUBWA : Kufundisha sala mbali mbali tunayofanya ndani ya Kanisa letu la JAMAA TAKATIFU.

1.- SALA YA BABA YETU : ifundishwe vile iko ndani ya Biblia (MATAYO 6:9-15).

" Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litakaswe, ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe siku kwa siku riziki yetu. Utusamehe zambi zetu kwa kuwa sisi nasi tumsamehe kila anaye tukosea. Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule muovu."

tunasema "Baba yetu uliye mbinguni", njo Mungu Baba Muumbaji, Mungu Mwana Mkombozi na Mungu Roho wa Mapendo. Sala hii ilifundishwa na Bwana Yesu Kristu.

Sala ya Baba yetu ina sehemu mbili :

a) Inasema kama tunapashwa kumsifu Mungu kila siku. Mapenzi yake yaenee ulimwenguni kote na watu wote watii. Yesu alisema kama tuombe Baba tukipitia kwake Yesu (YOANE 16:23).

b) Inasema kama sisi watu tunamuomba Mungu atupe yote yenyi kuwa ya lazima kwa maisha yetu, na atuhurumie makosa yetu na kututosha mu vishawishi: kumbe tujuwe kuhurumia wengine ili sisi pia tuhurumiwe na Mungu.

2.- SALA YA BIKIRA MARIA : Kwa maneno ilisema Malaika Gabrieli kwa Maria, ilikuwa maneno ya wao wawili (LUKA 1:26-38).

Tuombe hivi: "Maria Mtakatifu, mama wa Yesu, uliye mkanyanga Shetani kwa nguvu ya Mungu,
Uishi kati yetu kama vile pa Nazarethi, ukituombea daima kwa Yesu wako, atupe Uzima, Uzazi na Mapendo."

Mama Maria, yeye ndiye alishinda Shetani na ndiye aliunganisha mbingu na dunia. Alisema wazi alipofika kwa Elizabethi (LUKA 1:39-80). Kumbe haifai tena kumupa salamu ao kumwamkia "JAMBO" kila siku.

3.- SALA YA SIFA : Baba Mungu anastaili kusifiwa na kuaoudiwa hapa duniani.

Tusali hivi: "Sifa kwa Mungu juu mbinguni na amani duniani kwa watu wenyi mapenzi mema.
Tunakusifu, tunakuabudu na tunakushukuru."

(MATAYO 2:1-3).

Mungu aliaribu dunia, lakini aliihurumia; alifanya alama ya upinde. Tena akatoa Mwana wake wa pekee, Yesu Kristu. Kumbe hatuwezi kumuomba atupatie mambo ya zamani; yeye sasa ni wakutukuzwa tu, kusifiwa na kumshukuru kwa wema ule ametutendea.

ANGALISHO : MWALIMU afundishe watoto kusali na unyenyekevu.

SURA YA PILI : KUAMKIANA " J A M B O "

Kiini cha neno hili ni Uzima moja, Uzazi moja na Mapendo moja. Maana yake: tupo sasa wandugu wa mtu moja, tangu baba wa nyumba yetu pamoja na mama pia, bila kusahau mu Kanisa letu wale wote wababa na wamama tunakusanyika nao na kuonana nao. Ukiona baba ao mama fulani, umusalimie " JAMBO YETU", hata wa Kaka na wa Dada wetu na kati yetu pia. Kusimama na adabu pa kupana mkono kwa mkubwa.

1.- JAMBO YETU maana yake nini ?
2.- Wakati tunapokutana na baba, mama, kaka ao dada wa J.T.AF., tutamsalimia namna gani ?

x x

SURA YA TATU : KUJUA MAOMBI

* Kuomba ni kuzungumuza na Mungu, tukimtolea mawazo yetu.
Maombi si wimbo.
Mtoto mwenyi kuomba kwa baba yake kitu fulani anayoosha mikono kwa heshima.
Tunapoomba, mwili wote mzima na mawazo imuelekee Mungu kwa heshima na unyenyekevu.

* MWALIMU: usifundishe maombi marefu, bali mafupi (YOANE 14:13-14).
Panga maneno ya lazima muzuri.

MFANO: Tuombe - "Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho wa Mapendo: Tunakuomba utupe uzima, uzazi na mapendo, umoja wa kweli ndani ya nyumba yetu na mu Kanisa letu. Tunakuomba hayo tukipitia katika majina matatu matakatifu : ya Mungu Baba Muumbaji, ya Mungu Mwana Mkombozi na ya Mungu Roho wa Mapendo-Amen."

- "Mungu, tunakuomba sisi watoto tuwe mfano wa Yesu aliyekuwa mtii kwa wazazi wake. Na sisi tutii wazazi wetu. Tunaomba hayo tukipitia katika majina matatu matakatifu : ya Mungu Baba Muumbaji ya Mungu Mwana Mkombozi na ya Mungu Roho wa Mapendo - Amen."

Mara maombi yakiwa marefu, yawe hasa kwa wale wa miaka kumi; wao wanaweza kutaja ao kuongeza mawazo mengine mbali mbali.

1.- Ombi ni nini ?
2.- Tutaomba na hali gani ?

* * *

SURA YA INE : ADABU NA HESHIMA

- Mtoto mzuri ni yule mwenyi kusalimia wazazi wake nyumbani pa kuamka. Tunastahili vile vile kuamkia wageni wenyi kutufikia nyumbani mwetu.
- Sisi wakristu, tuheshimu jina la Mungu, wakubwa wa Serkali, wakubwa wa Kanisa letu, mwili wetu, mawazo ya Mungu tunayopokea na watu wote wasio wa nyumba yetu.

- Adabu inapashwa kuonekana wakati tunapokula, tunaposalimia watu, tunapokea Kanisani ao fasi ingine, na tunaposhauriwa na kupokea vitu m ali mbali tunavyopewa, tukisema AKSANTI.

MIFANO :-Matusi, upuuzi ao kuimba pa kula, kutembea tembea na kugusa vitu mbali mbali ndani ya nyumba isiyo yenu ni kukosa adabu.

-Kuvaa vibaya, makelele Kanisani na mu mafundisho, kukosa kuamkia watu na vivi hivi ni kukosa heshima.

1.- Kuchekelea mzee ao kilema anayepita njiani ni adabu ?
2.- Mkubwa akikukataza fujo bila sisi kusikia tunafanya nini ?
3.- Mtoto mwenyi adabu atafanya nini na wazazi wake ?

ANGALISHO: Kufundisha kuheshimiana na kulinda adabu katikati yao.

* * *

SURA YA TANO : KUACHA MAWAZO YA GIZA

Watoto kiisha kuwa na umri wa miaka nane hadi kumi wanaanza kuwa wezi, waongo, wasemaji wa kila neno na wenyi kujua kuficha vitu mbali mbali ndani ya nyumba. Tangu miaka kumi na kuendelea, wanajuwa ubaya wa dunia na akili inapanuka.

Wewe MWALIMU ao KIRONGOZI, anza kuwafasiria maisha ya Bwana Yesu: hakuiba hata siku moja; na wewe mtoto, kama unapenda wazazi wako, usiwaibe kitu; ukiona ao kuokota kitu nyumbani, uwaonyeshe na kuwapa.

1.- Mama anakutuma kununua sukari, njiani unalambula yote: unafanya nini ?
2.- Wakati anaaga ya kama unakwenda ku répétition ya nyimbo, lakini usifike ku nyimbo yenyewe, unafanya nini ? ao unatumia nini ?

ANGALISHO: Inafaa kutaja mfano wa watoto wezi wenyi unajuwa.-

+++

## SURA YA SITA : WATOTO WAJUWE KUSALISHA WAO WENYEWE

+ Kwa jina ...
+ Baba yetu X 1
  - Wimbo ...
  - Maombi ya mtoto moja ...
+ Maria X 1
  - Wimbo ...
  - Maombi ya mtoto moja ...
+ Sifa X 1
  - Wimbo ...
  - Maombi ya mtoto-moja ...

Pa nafasi hii, MWALIMU una kazi kubwa ya kuwasaidia nyimbo na kufuata kwa karibu maombi yao. Kama mtoto anatafuta kushindwa kuongeza maombi, wewe Mwalimu unaweza kumalizia maombi ile ya yule mtoto. Hivi watoto wengine wasipate kucheka wakati wa sala. Inafaa pia kupanga watoto wanaojuwa kuomba vizuri.

+ + +

## SURA YA SABA : MAULIZO MBALI MBALI (MKAGUO)

1.- Nani atatusalia sala ya Baba yetu ? Ina sehemu ngapi ? Afasirie.
2.- Nani alikuwa wa kwanza kusali sala hii ?
3.- Malaika gani alimwamkia Maria ?
4.- Bikira Maria ni nani ?
5.- Tunastahili nini kwa Baba Mungu ?
6.- Tunastahili kusalimia watu wote wa dunia JAMBO YETU ?
7.- Tunastahili kuwa na haya kwa kusalimia baba, mama, kaka ao dada wa J.T.AF. JAMBO YETU ?
8.- Sababu gani tunamutaja Mungu katika maombi yetu ?
9.- Kila mara tunaposali, tunaomba kwa nani ?
10.- Wakati tunamutukana kaka, dada, baba ao mama yetu, tunafanya nini ?
11.- Baba anaacha Z 1,00 pa meza; wewe unaibeba: unafanya nini ?

SURA YA NANE : KUCHUNGUZA WATOTO WA FUJO

Mtoto mwenyi fujo, umupe kazi ya kusalisha kila mara, usimuachie fasi. Unapashwa kumfuata kwa karibu sana yule afasirie mawazo ya juma iliyopita. Wakimaliza kufasiria, wewe Mwalimu fasiria na kuwaonya maneno ya :

- UZIMA : maana yake mtoto asiyeharibika katika matendo yake.
- UZAZI : maana yake mtoto mwenyi kufuatana na wenzake wanamzaa katika hali, tabia, juhudi, . .
- MAPENDO: maana yake mtoto wa roho mzuri, mufurahivu mbele ya wenzake, hasiye na hasira kila mara, anaye mtakia mwenzake heri na amani.

Japo kule juu tulitenga namna ingine, kwa wao kusikia, sherti kuweka hivi. Wajuwe kama kuwa uzima ni hivi, uzazi ni hivi na mapendo ni hivi.

*

* *

*

SEHEMU YA PILI

M A F U N D I S H O   Y A   V I J A N A
(tokea miaka 14 na kuendelea)

SURA YA TISA : WITO WA SAMWELI

Hivi wapate kujua kama wanaitwa na Mungu kusudi wapate moyo wa kuuliza wazazi kufanya hivi ni nini ? Kuwaelekeza sana kwa wazazi, vile Samweli alikwenda kwa Eli (I SAMWELI 3:4-17). Kuzidi kuwaonyesha kama Yesu alipenda sana watoto (LUKA 18:15-17).

\+ \+ \+

SURA YA KUMI : UKOMO WA "JAMBO YETU "

Kama vile mawazo tulisema mwanzo, ukomo wa "JAMBO YETU " ni kuwa kitu kimoja. Ni bora zaidi watoto wajulishwe kama tuko wana wa Mungu (WARUMI 8:14-17). Tena wajulishwe kama kwa kuwa tuko Kabila moja ya Mungu, nja maana tunasalimiana "JAMBO YETU." (YOANE IO:I5-I8).

+++

## SURA YA KUMI NA MOJA : IMANI YA KUMJUA YESU

Yesu ni Mungu wa kweli. Kwa kuwajulisha, sherti kufafanua sana kitu kile wanajua. MATAYO 2I:I8-22 : mti ulikauka ili mitume wapate kusadiki; wakati wa kurudi kwao, walipoona mti wenyi kukauka, wakasadiki kama Yesu ni Mungu; MARKO 4:35-41 : Yesu anatuliza bahari.

MWALIMU : Uwe unaangalia kama waponasikia ao hapana, kusudi waelee ya kama Imani ya kweli ni kujua kama sisi wote tuko na mkummoja hapa duniani.

../..

## SURA YA KUMI NA MBILI : MATUMAINI

Kutumaini Mungu: Kwa kuwajulisha wazo lile, sherti wewe Mwalimu uwaelekee sana, nao wakitambua vile kama unawaelekea, ni kwepesi sana nao kusikia mafundisho ya matumaini. Tena kuwaonya vema kama Mungu hapendi ubaya: ukiwa na ubaya, Mungu hatakuangalia (WAROMA I2:I7-2I).

oOo

## SURA YA KUMI NA TATU : UTII

Mtoto mwenyi kutumaini kwa Mungu atamjua Mungu, hasa wakati anatii wazazi wake nyumbani.

MWALIMU: hapa uzidi kuwaonya zaidi juu ya utii (I PETRO 5:5-11).

Tena Mtoto anaombwa kukubali ao kupokea mafundisho ya wazazi kusudi apate Hekima kubwa na Maarifa (MEZALI 1:8; 14:16).

ooOoo

## SURA YA KUMI NA INE : MAPENDO

Mtoto mwema anapenda baba na mama ku nyumba. Wakati anapopenda wazazi wake, anampenda Mungu. Onya kwa Mapendo Mungu alitupenda: alikufa msalabani kusudi ya kutukomboa ku utumwa wa zambi; amejitolea mzima (I YOANE 4:7-2I).

MWALIMU: Uzidi kuonyesha wazi kama mtoto mwenyi kujitolea kila mara kwa kuishi karibu na wazazi atakuwa na baraka kubwa.

.../...

SURA YA KUMI NA TANO : JAMAA NI NINI ?

Ni kundi la wakristu wenyi kufuata mawazo tatu ya Mungu iliyopotea : Msikilizano, Msaidiano na Mapendo.
MWALIMU aeleze maana ya kundi; kuwaonya wazi wazi vile makundi iko mu dunia ya kila namna. Na kundi letu ni kundi la namna gani ? Maelezo ya hapa yadumu hata mwezi mzima, kusudi wajue kama makundi yote siyo makundi ya Mungu.

.../...

SURA YA KUMI NA SITA : MAWAZO MATATU

Vile tuliona mwanzo, kuna wazo la Uzima, Uzazi na la Mapendo. Sasa vijana wapewe mawazo ya Msikilizano, Msaidiano na Mapendo. Kuifafanua siku mbali mbali:

- Kuonyesha Msikilizano wa Jamaa na ule wa vikundi vingine vya ulimwengu.
- Kuonyesha Msaidiano.
- Kuonyesha Mapendo.

O•oo•OooooO

SURA YA KUMI NA SABA : MKAGUO

- Kila mara MWALIMU atoe mafundisho mafupi, iwe inadumu muda usio-murefu: isipite dakika 30 ao 40.
- Kila mara Mwalimu atoe maulizo kiisha kuwafundisha sehemu, kipindi ao sura fulani muda wa juma mbili ao tatu, mbele ya kuongeza fundisho lingine.
- Tena Mwalimu awe nasoma masomo kama haya:

| | |
|---|---|
| I SAMWELI 3:4-I7 ; | LUKA I8:I5-I7 |
| YOANE IO:I4-I8 ; | MARKO 4:35-4I |
| WARUMI I2:I7-2I ; | I PETRO 5:5-II |
| I YOANE 4:7-2I ; | MATAYO 25:1-13 ... |

- MWALIMU anaweza kufundisha pia watu wazima.-

-/-

SURA YA KUMI NA NANE : DAUDI ANAPAKALIWA MAFUTA

MWALIMU awaonye Vijana wapate kujua kama Daudi alikuwa mtoto sawa wao; Mungu alimchagua na akapakaliwa mafuta na Samweli ili awe mfalme wa Israeli. Aliokoa Israeli katika mikono ya waadui na hata akamshinda Goliati kwa nguvu ya Mungu (I SAMWELI I6:6-I3; I7:1-11; 32-39; 40-54).

MWALIMU awaonye juu ya kuokoa nyumba yao. Tena wategemee Mungu na kushinda Shetani (Goliati); wajuwe kama Mungu hachaguwe kimo ao umri, ila moyo safi.-

(.....)

SURA YA KUMI NA TISA : MATESO YA AYUBU

Ayubu, mtu wa imani, alitumainia Mungu. Kiisha kupata mali mingi, alijaribiwa na Shetani: alipata mateso makali ya majipu na kupotelewa na mali yake yote (AYUBU 1:1-22; 33:1-33).

Ayubu alikataa mashauri ya bibi yake na warafiki; alijua kama mwenyi uzima wote ni Mungu.
MWALIMU awaonye Vijana na awapatie moyo wa kuvumilia mateso ya dunia sawa vile Ayubu; wawe na Imani na matumaini kwa Mungu; wajuwe kushindana na Shetani kwa sala; watambue Shetani katika watu wanaoishi nao.-

(.o+o.)

SURA YA MAKUMI MBILI : IMANI YA IBRAHIMU

Ibrahimu ndiye anayeitwa baba yetu kwa njia ya Imani. Alikubali sauti ya Mungu, akaondoka katika inchi yake ya kuzaliwa na kwenda ku inchi ya kigeni ili afunge Agano na Mungu. Aliacha vyote (mali yake).

MWALIMU ajulishe Vijana habari hii, ili watoke mu tabia ya zamani na kuingia mu tabia ya Bwana Yesu; wakubali sauti ya Mungu, hivi wafunge naye Agano, waache matendo yao yote mbaya (MWANZO 12:1-7).

* * *

## MAJIBU YA MAULIZO JUU YA MAFUNDISHO

Tuangalia :

- Sura ya kwanza :
    1.- JAMBO YETU ni kutakiana Uzima, Uzazi na Mapendo katika maisha yetu. Kumbe sisi wote ndani mwa Kristu tuko wandugu.
    2.- Wakati tunapokutana na baba, mama, kaka ao dada wa J.T.AF., tutamsalimia JAMBO YETU.
- Sura ya tatu :
    1.- Ombi ni kuomba Mungu Baba kwa jina la Mwana wake Yesu Kristu atupe sisi vitu tunavyohitaji, na kuweka mbele yake maneno mbali mbali mengi tunayotaka aifanye kwa sisi na kwa watu wengine.
- Sura ya ine :
    1.- Tukicheka Mzee ao kilema anayepita njiani tunakosa adabu na hatatupa razi.
    2.- Watu wanapotukataza fujo sisi hatusikii, tunakosa adabu na tunawazarau tu, si vizuri. Twastahili kusikia shauri la wakubwa a wenzetu wakati wanapotushauria.
    3.- Mtoto mwenyi adabu anasikia kila shauri ao neno jema la wazazi wake, kuwasaidia katika maisha yao nyumbani na kila siku kuwaamkia asubui na kuamka, kuwaaga pa kwenda fasi fulani ao pa kulala.
- Sura ya tano :
    1.- Wakati unalambula ndiazi sukari yenyi ulitumwa na mama kununua, umeiba.
    2.- Wakati ule unatumia uongo na uko mtoto wa Shetani kwa kuwa umeaga ya kama unaenda ku répétition ya nyimbo, lakini haukufike ku nyimbo yenyewe.
- Sura ya saba : MAJIBU YA MAULIZO YA MKAGUO :
    1.- Sala ya Baba yetu ina sehemu mbili (angalia mafasirio yake).
    2.- Aliyekuwa wa kwanza kusali sala hii ni Mungu Mwana, yule aliyetukomboa, Bwana wetu Yesu Kristu.

3.- Malaika aliyemwamkia Maria ni Malaika Gabrieli.

4.- Bikira Maria ni mtoto wa Yohakimu na Ana, yeye aliyejaliwa neema na Mungu Baba, akapata mimba kwa nguvu ya Roho Mtakatifu wakati alipokuwa mchumba wa Yozefu Mtakatifu, na ni Mama wa Mungu, aliyemzaa Bwana Yesu.

5.- Kwa Mungu Baba, tunastahili kumsifu, kumuabudu na kumshukuru.

6.- Hapana, hatustahili kusalimia watu wote wa mu dunia JAMBO YETU, mpaka wale tunao mu J.T.AF.

7.- Hapana, hatustahili kuwa na haya kwa kusalimia baba, mama, kaka ao dada wa J.T.AF. "JAMBO YETU."

8.- Tunamutaja Mungu katika maombi yetu kwa sababu ni yeye mkubwa wa vitu vyote aliyeumba mbingu na dunia, uweze wote ni wake, sisi tupo mali yake.

9.- Kila mara tunaposali, tunaomba kwa Baba Mungu.

IO.- Wakati tunamutukana kaka, dada, baba ao mama yetu, tunakosa adabu na heshima.

II.- Kama baba anaacha Z 1,00 pa meza na wewe unaibeba, unafanya wizi.-

MAULIZO JUU YA WACHUMBA PAMOJA NA MAJIBU YAKE

1.- Kwa sasa, hivi munakuwa pamoja, muko watu wangapi ?
J/ Tunakuwa mtu mmoja (MATAYO 19:4-6).

2.- Ni bibi gani aliyepewa mashauri mu kitabu cha MWANZO ?
J/ Ni Rebeka (MWANZO 24:58-60).

3.- MU nyumba kwa kubaki kimya, ni sherti kufanya nini ?
J/ Inafaa kupeana haki (WAEFESO 5:25-28).

4.- Kwa kukaa vema mu nyumba, ni sherti mufanye nini ?
J/ Ni sherti kupatana kwa kila njia (I WAKORINTO 7:3-5).

5.- Ni kitu gani kitafikisha watu ku nyumba yenu ?
J/ Ni utii wa mama (I PETRO 3:1-2).

6.- Mu nyumba yenu mutakuwa mutumwa ?
J/ Hapana, tutabebana sisi wote (I PETRO 3:7).

7.- Baba ndani ya moyo wa mama na mama ndani ya moyo wa baba, Mungu aliweka nini ? -J/ UZIMA (YOELI 1:4), UZAZI (MARKO 4:8-9) na MAPENDO (I YOANE 4:7-8).

ANGALISHO :

MWALIMU uwaonye watoto kama wasipoweza kutii shauri ya wazazi, Mungu anaweza kuwahazibu kwa sababu mzazi ni sawa na Mungu. Tena chini ya jua, haifai kuzarau mzazi ubwa wowote (WALAWI 20:9; 2 WAFALME 2:23-24; I SAMWELI 2:22-25; MEZALI 30:17).

Kumbe furaha ya mzazi ni mtoto mwenyi kuongoka na kuwa na heshima mbele ya watu woto (MUHUBIRI 7: ).-

* * * * *

KIPINDI CHA SITA

M A S H A U R I Y A W A Z A Z I K W A
U P A N D E W A W A T O T O

Kufuatana na Kanisa letu, tunapashwa pia sisi wazazi kujua kama tuna mzigo pia. Kumbe tunaombwa pia kuangalia watoto wetu. Haifai kusema tu kama hii miaka inageuka kwa upande wa watoto, hawasikie tena (MUHUBIRI 7:10-12).

Tena muangalie pia vile watoto wetu wekonakwenda ku kabumbu ao ku michezo fulani, wanazoea kukuaga na weko watii wakati unapowaambia kama muache kwenda kule, mufanye kitu fulani, kama vile Izaka aliweza kutii baba yake ? (MWANZO 22:6-9).

Kwa kawaida, ni vema pia kujikaza ili watoto wawe na Imani kama vile sisi wazazi tuko nayo (2TIMOTEO I:5). Kumbe hapainaonyesha kama Timoteo alikuwa na imani ile ile ilikuwa na wazazi wake (2 TIMOTEO 3:14-16). Kijana, Timoteo aliacha tabia yote kufuatana na nguvu ya wazazi (I TIMOTEO 6:11-12).

Kuwaonya watoto kujua Mungu, hii ni kazi ya wewe mzazi: wajuwe kukataa kitu kibaya na kufanya kile cha kupendeza Mungu na watu pamoja na Mungu ametupatia (YOANE 3:34). Kumbe haifai kuona makosa ya watoto na kukaa kimya kama Eli (I SAMWELI 2:22-25;3:12-14).

Ni bora kuangalia uongozi wako kadiri uko natoa amri nzito kwa ajili ya watoto (MEZALI 29:16). Hakuna mzazi hata mmoja ataachwa kuulizwa juu ya kazi yake na Mungu (I PETRO 1:17; ITIMOTEO 5:8).-

* * *

* * * * * * * * *

* * *

## Y A L I Y O M O

KICHWA CHA MANENO ........................................ UKARASA


UTANGULIZI .................................................1

INGILIO ....................................................2

KIPINDI CHA KWANZA

IMANI YETU NI GANI ?

Sura ya kwanza :Imani yetu ni Yesu na Maria ................3

Sura ya pili: Alama ya msalaba na sala .....................4

Sura ya tatu : Majifu na matawi ............................5

Sura ya ine : Uzima - Uzazi - Mapendo ......................6

Sura ya tano : Mtu ni mfano wa Mungu .......................7

Sura ya sita : Imani na maisha mapya .......................8

Sura ya saba : Kuamini kwetu ...............................8

Sura ya nane : Ujitazame kama una Imani ....................9

Wazo la mwisho .............................................9

KIPINDI CHA PILI

MAFUNDISHO YA UBATIZO

Ingilio .................................................... IO

Msikilizano ................................................ 11

Msaidiano ..................................................11

Mapendo ....................................................12

Mashauri ya Hekima :

- Utangulizi ...............................................13
- Maonyo mbali mbali .......................................13
- Mwenyi akili na mjinga ...................................14
- Matunda ya haki na ya uovu ...............................14
- Tafauti kati ya akili na ujinga ..........................14
- Hekima ya mtu mzuri ......................................14
- Mafundisho kwa mtu wa Mungu ..............................15
- Kazi yenyewe : a)-Kuumbwa kwa ulimwengu ..................15
  b) Edeni .................................................16
- Ubatizo ni tendo la tangu zamani .........................16

- Kutubu na Imani vinatembea pamoja ....................17
- Kwa kupokea Uzima wa milele ........................18
- Malaika ni mjumbe wa Mungu ........................18
- Malaika wabaya ......................................18
- Pepo wachafu wataishi ndani ya mwili wetu ..........19
- Mwenyi kupinga Kristu ...............................19
- Imani ni nini ? ..................................... 20
Imani iko inatufikia toka kwa Mungu namna gani ? .......20
Tunaweza kupokea Imani namna gani ? .................. 21
Mawazo yenyi kuzuia Imani ............................ 22
Imani inaleta nini ? ..................................21
Maulizo juu ya kipindi cha kwanza na cha pili ..........22
Maulizo ya Hekima ......................................22
Maulizo juu ya kuumbwa kwa ulimwengu ...................23
Ubatizo - Zambi - Malaika - Mpinga Kristu .....23
Maulizo juu ya Imani ...................................24

KIPINDI CHA TATU

MAFUNDISHO YA KOMUNYO YA KWANZA

Juma ya kariou na Komonyo ...............................25
- Kutubu kwenyewe ni nini ? ..............................25
- Kutubu kunaleta nini mu maisha ya wewe mwamini ? ..........26

KIPINDI CHA INE

MAFUNDISHO YA UCHUMBA

Uchumba .................................................27
Umtu ....................................................29
Mafundisho ya Ndoa ......................................30
Maelezo juu ya Ndoa .....................................31

KIPINDI CHA TANO

MAFUNDISHO YA WATOTO WADOGO NA VIJANA

Shauri ..................................................32

SEHEMU YA KWANZA

MAFUNDISHO YA WATOTO WADOGO (miaka 6 mpaka 13)

Sura ya kwanza ..........................................33
Sura ya pili : Kuamkiana."JAMBO YETU " ..................34
Sura ya tatu : Kujua maombi ..............................35
Sura ya ine : Adabu na Heshima ...........................35

Sura ya tano : Kuacha mawazo ya giza ........................36
Sura ya sita : Watoto wajuwe kusalisha wao wenyewe ............37
Sura ya saba : Maulizo mbali mbali (Mkaguo) ..................37
Sura ya nane : Kuchunguza watoto wa fujo .....................38
SEHEMU YA PILI
MAFUNDISHO YA VIJANA (Tangu miaka 14 na kuendelea)
Sura ya tisa : Wito wa Samweli ...............................38
Sura ya kumi : Ukomo wa "WIMBO YETU" .........................38
Sura ya kumi na moja : Imani ya kumjua Yesu ..................39
Sura ya kumi na mbili : Matumaini ............................39
Sura ya kumi na tatu : Utii...................................39
Sura ya kumi na ine : Mapendo ................................39
Sura ya kumi na tano : Jamaa ni nini ? .......................40
Sura ya kumi na sita : Mawazo matatu .........................40
Sura ya kumi na saba : Mkaguo ................................49
Sura ya kumi na nane : Daudi anapakaliwa mafuta ..............41
Sura ya kumi na tisa : Mateso ya Ayubu .......................41
Sura ya makumi mbili : Imani ya Ibrahimu .....................41
Majibu ya maulizo juu ya mafundisho ..........................42
Maulizo juu ya wachumba na majibu yao ........................43
Angalisho ....................................................44
KIPINDI CHA SITA
MASHAURI YA WAZAZI KWA UPANDE WA WATOTO ......44
Y A L I Y O M O ..............................................45

NYK.